

Mlango Mi Mwembamba

 Asante, Ndugu Neville. Asante. Ni vizuri sana kurudi Nyumbani mwa Bwana. Sikuzote mimi hufurahia kurudi kwenye Maskani, haidhuru popote niendapo. Kuna jambo fulani kuhusu mahali hapa padogo pa kale ninapopenda kuparudia. Ni tu, loo, mimi. . . Lilikuwa kanisa langu la kwanza na la pekee nililowahi kuwa mchungaji wake. Na inaonekana jema tu kurudi hapa tena. Nami naamini kwamba panapo asubuhi ile kuu jua litakapokataa kuangaza na nyota kufifisha nuru yao, naamini kutakuwa na baadhi kutoka maskani hii watakaokuwepo siku hiyo, ambao wameoshwa katika Damu ya Mwana-Kondoo. Nautazamia wakati huo.

² Nilipokuwa nikija kupitia chumbani hivi sasa, nilikutana na Dada Arganbright kule nyuma. Naye alikuwa akiniambia kwamba kulikuwa na baadhi ya watu hapa ambao walikuwa kwenye mkutano wa Kingston, ambao walizuru wakati huo, nami. . . ule. . . nina furaha sana kuwa nao hapa kama ushuhuda. Popote walipo, kama watainua mikono yao, walikuwa kwenye mkutano wa Kingston huko Jamaica. Hebu, naam, nyuma pale nyuma. Vema, hilo ni sawa.

³ Naona postikadi ya Oral. Nadhani mmekwisha tangaza mikutano yake. Sikujua mpaka, hizo tarehe, mpaka jana. Nafikiri inaanza tarehe sita, sivyo? Tarehe sita hadi kumi na tano, Ndugu Roberts huko Louisville. Sasa, nendeni mkamsikilize. Ndugu Roberts ni rafiki yangu m—mpendwa, na mtumishi halisi wa Kristo. Nami nina hakika mtafurahia jumbe zake, usiku baada ya usiku. Na. . . yake, wakati anapowaombea wagonjwa, nina—nina hakika kwamba mtamwona Mungu akitenda kazi, kwa sababu yeye ni shujaa mkuu wa imani, Ndugu Roberts ni shujaa, na mtu ambaye Mungu anamtumia sana. Na huduma yake imepanda kutoka. . .

⁴ Nakumbuka wakati nilipokutana kwanza na Ndugu Roberts, alikuwa katika hema dogo lililochakaa huko St. Louis, Missouri, nami nilikuwa. . . la, Jiji la Kansas, Missouri. Nami nilikuwa katika Jiji la Kansas, Kansas, katika jumba la mikutano. Aliketi kwenye kiti cha mbele. Baada ya ibada kwisha, tulizunguka nyuma na tulikuwa tukiongea. Walinijulisha kwake. Ana umri mdogo kuliko mimi; Oral yuko katika miaka yake ya arobaini ya mwanzoni. Na hivyo akasema, “Unafikiri Mungu angesikia maombi yangu kwa ajili ya wagonjwa?”

Nikasema, “Ndugu, Yeye atasikia maombi ya mtu yeyote ambaye ataomba.” Vema, akaanza kuondoka, naye akasema, “Mimi hapa naenda!”

⁵ Naye ni mtu mwerevu sana, na elimu ya chuoni, miaka minne ya saikolojia, na nina hakika yeye ni—yeye ni mtu mwenye akili sana. Na amefikia mahali sasa ambapo amezungukwa na kundi la washauri, na kadhalika, mpaka, anaponena, hu—huyawazia maneno. Nanyi mtamfurahia kweli, nina hakika.

⁶ Na kwa hiyo sasa ningetaka kutoa taarifa ndogo tu juu ya yale Bwana wetu amefanya katika mkutano wetu mdogo mnyenyekevu huko Jamaica na Puerto Rico. Lilikuwa jambo la ajabu kwamba nilikwenda, kwa sababu simu nyingi zilipigwa. Kama Leo hapa anavyofahamu, kwamba simu... Na katika kipindi cha juma moja, kuna yapata mahali mia kadha hupiga simu kwa ajili ya mikutano. Lakini hata hivyo napenda kusikia nikiongozwa niendako, kama ilivyokuwa kwa huo. Kama nikienda kwa sababu mtu fulani ameniagizia nije, basi ninakuja katika jina la hilo kanisa au shirika hilo. Kama ningenda kwa sababu Ndugu Neville alisema yanipasa niende, ingenipasa kwenda kwa jina la Ndugu Neville. Lakini nataka kwenda wakati Yesu anapotuma, kwa hiyo unaweza kwenda katika Jina la Bwana Yesu, kukutana na watu.

⁷ Nami nilikuwa nimelala kitandani, na nilikuwa nimechoka kidogo. Bonde hili, siku moja, itanibidi kuondoka kwenye bonde hili, kwa sababu linakausha koo langu sana hata ni vigumu kwangu kulivumilia. Naweza kuondoka na kurudi... Tulikuja hivi majuzi, mimi na Leo, yapata maili arobaini, baada ya kuwa katika vinamasi huko Florida, koo limepona kabisa, na yapata maili arobaini kutoka Louisville likakwama tena. Ndugu Banks Wood anapaswa kuwa mahali fulani hapa asubuhi hii. Na hivi majuzi nikija kutoka Kingston na—na Puerto Rico, ambako koo langu lilikuwa sawa kabisa; na nilishuka kutoka kwenye ndege, bado liko sawa; na kabla hatujafika Jeffersonville, likajifunga tena. Unaona, ni hili bonde hapa. Ni bakteria hewani, ama labda ni Mungu, mojawapo, akijaribu kuniiondoa hapa. Kwa hiyo, mimi—mimi sielewi jambo hilo. Nimeomba na kusihi mara nyingi sana.

⁸ Lakini, hata hivyo, nilikuwa ndiyo tu nimeamka, ilikuwa kama saa tisa alfajiri. Na mke wangu na mwanangu mdogo walikuwa wamelala. Nami niliinuka pembeni mwa kitanda, kisha nikaona watu wengi mno walikuwa wamekusanyika mahali pakubwa, nami nikamwambia Billy Paul, “Nenda kule ndani uwape watu hao kadi za maombi.”

⁹ Naye akasema, “Sawa, baba.” Mnamo dakika chache akarudi, akasema, “Huwezi kuwapa watu hao kadi za maombi.” Akasema, “Unamwona mtu huyu anayesimama hapa?”

Nikasema, “Ndiyo.”

¹⁰ Akasema, “Alikuwa hapa, nami nikasema, ‘Kila mtu anayetaka kadi ya maombi, inueni mikono yenu.’” Akasema, “Nilikwenda kumpa kadi ya maombi, akaenda mahali pengine.

Na kisha nikaenda huko, naye alikwisha kwenda mahali pengine. Sasa, huyu hapa amerudi hapa.” Akasema, “Siwezi hata kutoa kadi moja ya maombi.”

¹¹ Nikasema, “Vema, Billy, haitakulazimu kutoa kadi za maombi, kwa sababu pana nafasi kubwa sana hapa hata kila mtu anaweza. . .” Kadi za maombi ni kuzuia ghasia. . . unaona, na kuwaweka katika utaratibu. Nikasema, “Loo, naweza kuchukua kila mtu hapo, hawazidi walioko katika nafasi niliyo nayo, na kuwafanyiza mstari na kuwaombea mmoja mmoja.”

¹² Naye akasema, “Sawa.” Naye akageuka upande wa kuume na kuniondokea. Nami nikageukia upande *huu* alipoelekea upande *ule*, na nilikuwa nikimwangelia.

¹³ Ndipo nikasikia Sauti ikishuka kutoka Mbinguni, ikasema, “Lakini wakati huu nitaanza kukutukuza.” Nami nikatazama, na kamwe sijawahi kuona halaiki kama hiyo ya watu, walikuwa wanasongamana kutoka kila mahali.

¹⁴ Na jina la Ndugu Roberts liliitwa, kasema, “Sasa Ndugu Oral Roberts anakuja kukuona.”

Nami nikasema, “Nitamsalimia namna gani Ndugu Roberts?”

Kasema, “Jinsi atakavyokusalimia.”

¹⁵ Vema, nilimwona Ndugu Roberts akija amevaa suti nyeusi, na kofia ndogo kama avaayo Bing Crosby, zile ndogo za kupindua juu na kuvuta chini, kofia ndogo nyeusi. Nami kwa namna fulani nilikuwa nimesimama, naye akainua macho akasema, “Halo, Ndugu Branham.”

Nami nikasema, “Halo, Ndugu Roberts,” nikampa mkono.

Akasema, “Una kundi zuri.”

¹⁶ Nikasema, “Kundi kwelikweli, Ndugu Roberts.” Naye akageuka akaenda jinsi aliyoenda Billy, kuume.

¹⁷ Nami nikawaza, “Nitawazungumzia nikiwa wapi?” Nami nikajaribu kila mahali kupata mahali pa kuzungumzia. Nilikuwa katika hali ambayo, kitu fulani chini, hata sikuweza kuona mahali pa—pa kuwazungumzia.

Ndipo mtu fulani akasema, “Vema, njoo hapa.”

¹⁸ Nikasema, “Vema, usingeweza kuona vizuri zaidi hapo.” Nami nikaanza kwenda upande wa pili wa mahali pale. Kisha nikakumbuka jambo hili basi, nikasema, “Jambo muhimu nipaswalo kufanya ni kuwa mnyenyekevu moyoni mwangu, sikuzote, mbele za Mungu na watoto Wake.”

¹⁹ Ndipo nikatoka katika hilo ono. Nikawaza, “Hilo linamaanisha nini? Labda linamaanisha tutakuwa na jambo. . . Au itakuwa—itakuwa wapi?” Unaona, wakati mwingine, katika maono, Yeye hakuambii ni wapi hasa, Yeye—Yeye hunena tu na

wewe . . . Ni kama fumbo, kitu kama hicho. Na nina hakika ninyi mnaosoma Biblia mnaelewa hilo.

²⁰ Na kisha nikaenda katika chumba cha mbele na kuketi chini kwa muda kidogo, na ilikuwa kama saa tisa na nusu au saa kumi alfajiri. Nililemewa sana na usingizi. Nilirudi nikajilaza chini, na nikaota ndoto, nayo ilikuwa ndoto ya ajabu sana. Na karibu ninyi nyote mnamjua mmoja wa mameneja, Jack Moore. Ndugu Jack Moore, nimemjua kwa miaka mingi. Nilifikiri kwamba nilikuwa nimempa binti yake miadi, msichana wa yapata umri wa miaka kumi na saba, na nilikuwa nimemshika mkono, nikimwongoza kukwea kilima, mtoto Jackie. Vema, nimemjua tangu alipokuwa mtoto mchanga tu anayenyonya. Nami nilikuwa nikimwongoza kuelekea juu kilimani, na nilikwenda umbali wa majengo matatu ya jiji nikipanda kilimani, nikimwongoza msichana huyu. Ndipo tukafika chini ya mti mkubwa, naye akaketi chini. Na kama wengi wa wasichana matineja siku hizi wanavyovaa hizo sketi ambazo, mwajua, kwa namna fulani zimepanuka, naye alikuwa amevaa moja ya sketi za aina hiyo. Basi akachukua sketi hii ndogo na kwa namna fulani akaitandaza kisha akaketi chini. Na kama vijana kwa kawaida wanavyoangaliana, alikunja mikono yake *hivi* na kuanza kuangalia juu angani. Vema, Jackie ni maskini msichana mzuri sana, lakini ana kinywa kikubwa mno na macho makubwa mno, na nywele za changarawe hivi, si wa kuvutia sana, lakini maskini msichana mwenye heshima. Na niliweza kuona macho yake makubwa alipokuwa akiangalia juu, na jinsi uakisi wa anga ulivyokuwa machoni mwake.

²¹ Vema, nikaenda karibu futi tano toka kwake, na kwa namna fulani nikalala upande *hivi*, na nikachukua unyasi nikauweka kinywani mwangu, na kuanza kuutafua unyasi huu. Nami nikaanza kuwazia, “Hivi ninafanya nini hapa? Mbona, mimi mzee, nikiwa na huyu msichana mdogo. Mbona,” nikasema, “nimeoa na nina watoto kadha. Sina shughuli yoyote hapa na msichana huyu mdogo.”

²² Ndipo nikaanza kuinuka. Na, nilipoinuka, Sauti ikaja kutoka kwenye ule mti, ikasema, “Jambo hili ni kwa ajili ya ishara na kwa kusudi fulani.”

²³ Nami nikaamka, na karibu nipige yowe, ji—jinamizi. Nikawaza, “Loo, nashangaa kama hilo linamaanisha kwamba nitarudi nyuma au jambo fulani litanipata?” Vema, nikawazia, “Kama nikijaribu kutumia akili yangu, basi nitajitatanisha nalo kabisa, kwa hiyo nitamngojea tu Mungu.” Basi nikaanza kuomba. Nikasema, “Bwana, je, ndoto hiyo inahusiana na lile ono kwenye sehemu ya mwanzoni mwa usiku, au inamaanisha nini?”

²⁴ Baada ya kungojea kwa muda fulani, labda saa moja, (Mke wangu alikuwa tayari ameamka na alikwisha andaa

kiamshakinywa.), ndipo ile Sauti ikarudi tena, na kusema, “Nenda Kingston, na utaambiwa huko la kufanya.”

²⁵ Kwa hiyo, mara nikaenda Kingston. Na wao—wao walijua Alhamisi alasiri kwamba ningekuwepo kule Ijumaa. Hayo ndiyo matangazo pekee tuliyokuwa nayo. Mimi si mzuri sana wa kufanya...?...au kukadiria umati, kwa sababu kwa kawaida mimi hutia chumvi. Lakini usiku wa kwanza, ningesema tulikuwa na karibu kumi na mbili, loo, yapata watu elfu moja na mia mbili, nje, kwa sababu ulijulikana tu siku moja. Na siku iliyofuatia wakimbiaji wakaanza kukimbia maili nne, katika mbio za kupokezana, wakipanda milimani. Mkimbiaji mmoja angekimbia kwa masaa manne, ndipo anamwachia mkimbiaji mwingine apande juu mlimani. Basi usiku wa pili kulikuwa na kama elfu tano. Na usiku wa tatu ilikadiriwa kwenye elfu kumi na tano, labda ishirini. Na kulikuwa na maelfu mara maelfu waliomjia Bwana.

²⁶ Na lile ono lilikuwa, lile kanisa dogo, yule msichana alikuwa bikira, mtoto tu, na hilo lilimaanisha ubikira wa kanisa hilo. Na ule umbali wa majengo matatu ya jiji kuelekea juu kilimani, ulikuwa siku tatu ambazo ningehudumu. Na kulichukua kanisa hilo dogo bikira kwa huduma yangu, kutoka lilipokuwa, kuendelea juu zaidi katika mambo ya Mungu, hadi likatikisa kisiwa kizima.

²⁷ Na, loo, wahudumu na watu kote kote, wakilia na kusihi na kushawishi, “Usiku mmoja tu au mbili zaidi,” wakuu wa lile jiji.

²⁸ Tulitoka huko tukaenda Puerto Rico. Huko tukapokelewa kwa shangwe nyingi mno, na maelfu mara maelfu walijaa njiani, mpaka ilikadiriwa yapata watu wa thamani elfu arobaini walimjia Bwana Yesu. Na wakati wa kuondoka, natumaini ni...ningesema hili kwa kanisa langu mwenyewe, lakini singeweza kulisema nje hadharani, mahali ambapo hakuna watu wa nyumbani, kwa sababu lingeweza kuchukuliwa vibaya. Lakini ninalo jina la hakimu huyo hapa kwenye kijikaratasi, aliyetoa hotuba tulipokuwa tunaondoka, papa hapa, yeye na wasaidizi wake.

²⁹ Na yeye...A—alisema, “Tumejaliwa kisiwani kuwa na wahudumu mbalimbali.” Akasema, “Wakati Bw. Billy Graham ameondoka tu kisiwani hivi majuzi,” akasema “tulikuwa na m—mkutano wa kupendeza,” akasema, “lakini Billy Graham alituletea tu Injili ile ile ambayo tumesikia sikuzote.” Akasema, “Kisha tulijaliwa kumpata Bw. Roberts kisiwani,” akasema, “naye Bw. Roberts alitupa mkutano mzuri sana wa siku tatu. Lakini,” akasema, “gharama zilikuwa juu sana hotelini,” akasema, “aliacha dola thelathini na tano elfu kwa siku tatu, kwa gharama za hoteli.” Akasema, “Kisha Bw. Osborn alikuwepo hapa, ambaye alikuwa mtumishi mashuhuri wa Kristo. Lakini,” akasema, “wakati Bw. Osborn alipoondoka,

kulikuwa na hali ya kushushwa,” akasema, “ilionekana kana kwamba kila kitu kilikuwa kimetoweka.”

³⁰ “Lakini,” akasema, “tuliona katika mkutano huu kwamba ilikuwa vigumu hasa kumpata mtu yeyote kwenye jukwaa wa kuombewa na Ndugu Branham. Lakini,” akasema, “baada ya ibada kumalizika, tungeokota malori yaliyojaa viti vikuukuu na rungu na kila kitu, nje katika kusanyiko.” Akasema, “Haikuwa mwanadamu wakati huu, Mungu alitujia,” akasema.

³¹ Nikasema, “Msitarajie maombi yangu; lakini maombi yenu huko nje, wekeaneni mikono nyinyi kwa nyinyi.” Nao wangeleta labda dazani moja au mbili jukwaani, na, wakati upambanuzi uliposhuka, watu wangepiga tu mayowe. Tuliishi katika hoteli ya daraja la nne, na kulipa gharama zetu zote wenyewe na usafiri, sisi wenyewe.

³² Ulisaidia kufanya hilo, mwenyewe, kwa zaka zenu ambazo mnanitumia. Hizo ndizo zilizofanya hilo. Na nataka ninyi mjue kwamba, kutokana na yote hayo, mnayo sehemu ya jambo hilo. Na katika ile siku kuu tukufu ijayo, Mungu atawapa thawabu ya jambo hilo. Mnaona, haikuwalazimu. . .

³³ Kama mtu binafsi anakwenda na kufanya jambo fulani, basi, unaona, wakati mtu huyo anapoondoka, wanafikiria, “Kushushwa kubaya, Mungu ametuacha.” Mungu hawaachi. Yuko pamoja nanyi sikuzote. Mnaona, una sehemu katika jambo hilo kama yeyote, kama mtu yeyote yule. Mungu anaweza kumtumia mtu kwa huduma fulani, lakini hilo halimaanishi kwamba mtu huyo ana upendeleo kwa Mungu. Ni imani yako mwenyewe katika Mungu.

³⁴ Nao wangekwenda nje kule katika magari madogo makuukuu ya kukokotwa, ambayo wangechukua kama vile magurudumu madogo ya mkokoteni, na—na kuyatengenezea ubao, na kuwalaza watu juu yake na kusukuma wakawaingiza ndani. Na baada ya ibada kwisha, uwanja wote ungekuwa wazi, wangekwenda tu na mabehewa na kukusanya mikokoteni midogo mikuukuu na viti vikubwa vikuukuu, na marungu na virago na vitanda, na papo hapo tu ambapo walitoka na kuviacha, kwa sababu Uwepo wa Bwana ulikuwepo pale. Hilo ndilo tunalotaka kuona. Binadamu haonekani wakati huo, Mungu anatenda kazi.

³⁵ Nikirudi, kusaia tu sasa asubuhi hii, nitazungumza kwa dakika chache. Nami niliwaomba vijana wasiitoe kanda hii. Siku tatu nimejaribu sana kufikiri, “Nitazungumza juu ya nini?” Na asubuhi hii, kabla ya kuondoka, nilihisi onyo kali sana moyoni mwangu kwa kanisa. Nami nikawaambia, “Rekodini kanda, lakini msizitoe zikauzwe.”

³⁶ Lakini kabla hatujafanya hili, ningetaka kuwapa ushuhuda mdogo tu, ili uweze kuwasaidia. Ulinisaidia. Tulifanya ziara ya siku tatu ya kuvua samaki, mimi na Leo na Gene, na mwanangu

Billy Paul na mkewe, huko chini kwa rafiki ambaye huhudhuria hapa maskanini, kutoka huko Georgia. Nao walitrudisha kwenye kinamasi fulani, sijui ilikuwa ni wapi sasa, karibu na Okeechobee au kitu kama hicho, sijui hao Wahindi wa Seminole wanapaitaje. Lakini, hata hivyo, tulikuwa maili nyingi kule nyuma.

³⁷ Na huyu Ndugu Evans, ndugu yake ni mwenye dhambi. Naye ni mvuvi mashuhuri, naye alirudi huko kwenye vinamasi miezi michache iliyopita. Na wana kile wanachokiita “mchacharika wa ardhini.” Ndipo nyoka mchacharika wa ardhini akamuuma, naye aliponea chupuchupu. Mguu wake ulivimba, na wakampeleka kwa madaktari na wakamdunga sindano. Viumbe hao ni wa kufisha. Na wana nyoka wengi wa majini wenye sumu nyuma huko pia, nyoka wa majini mwenye sumu, nyoka mkali kama pili, mamba wenye urefu upatao futi ishirini.

³⁸ Na tulipokuwa tunavua samaki nyuma kule, nilikuwa nimemnasa samaki mkubwa mno. Loo, ilikuwa siku ya—ya mapumziko kweli. Na alikuwa mkubwa sana hata sikuweza kumtoa majini, na aliinyosha tu ndoana na akaenda zake, au akavuta na kujinasua. Na tulipata samaki wengi, yapata ratili mia moja na hamsini za samaki wakubwa. Na hao, baadhi yao wakiwa na uzito wa ratili kadha wa kadha, na kutoka ratili nne hadi saba, ratili nane. Nami nilimshika huyu mkubwa, kisha akaponyoka.

³⁹ Ndipo nikarusha tena, na ni—nikamkamata mwingine, yapata ratili sita, saba. Na nilikuwa na ufito mrefu ambao ilikubidi kushikilia juu ya majani ya yungi. Naye Ndugu Evans alikuwa... Sote tulikuwa tumelowa kutokana na kutembea kwenye maji, kwa sababu kote ni majimaji tu. Naye alikuwa amevua viatu vyake na kukunja miguu ya suruali yake, na alikuwa ameketi mahali padogo pakavu, kidogo akikausha nguo zake. Naye akaona samaki huyu mkubwa akigaagaa katika vichaka, nami nilikuwa ninapita katika matope kumwelekea. Akasema, “Hebu kidogo, Ndugu Branham, nitakushikia huyo.” Naye akakimbia kule. Nami nilikuwa nimemvuta, nafikiri huyo samaki alikuwa karibu amekufa, akiwa amelala katika majani ya yungi. Naye akatoka akikimbia kumwokota. Ndipo, wakati alipofanya hivyo, alilia kwa uchungu, naye huyu hapa akarudi. Nyoka mchacharika alimwuma.

⁴⁰ Nasi tuliuangalia, na palikuwa na matundu ya meno ya nyoka katika mguu wake mahali ambapo yule nyoka mchacharika alikuwa amemwuma, na ulikuwa unamwuma sana mpaka machozi yalikuwa yakimlengalenga. Kasema, alijisikia kama kwamba mifupa yake ilikuwa inapooza. Na sisi hapo, maili nyingi nyuma kule katika kile kinamasi. Yeye ni mtu mnene sana hatungeweza kumbeba. Na wakati nyoka anapokuuma, unakuwa mgonjwa sana katika dakika chache

mpaka unakuwa karibu kufa. Na Leo alikuwepo amesimama. Ndipo kitu kikanijia akilini, “Wewe ungali ni Mungu!” Na wakati alikuwa akishikilia mguu wake na kuushika kwa nguvu, na yale matundu makubwa mawili ya meno ya nyoka hapo ambapo yule mchacharika alimvamia, niliweka mikono mahali hapo na kusema, “Bwana, imeandikwa katika Neno Lako, ‘Watakanyaga vichwa vya nyoka na nge, na hakuna chochote kitakachowadhuru kamwe.’” Na wakati uo huo, kila maumivu yaliondoka kwenye mguu wake. Akavaa viatu vyake na kuvua samaki siku nzima.

⁴¹ Tulikwenda usiku huo na kuwasimulia hilo, wakasema, “Heri uende kwa daktari.”

⁴² Akasema, “Ikiwa Mungu amenilinda umbali huu, Yeye ataendelea kunitunza daima.” Tulivua samaki siku tatu, pasipo matokeo mabaya hata kidogo.

⁴³ Mungu angali ni Mungu. Yeye hutimiza kila ahadi. Na katika huduma yangu yote, hiyo ndiyo mara ya kwanza niliyowahi kumwona Mungu akija kwenye tukio la kuumwa na nyoka, kwa sababu ilikuwa mara ya kwanza niliyowahi kupata nafasi ya kumwomba mtu aliyeumwa na nyoka. Ni kukujulisha tu kwamba Yeye hutimiza ahadi Zake zote, na Maneno Yake ni mema na ya kweli. Amina.

⁴⁴ Kumbukeni ibada usiku wa leo na Jumatano hii ijayo. Na mumwombee mtu sasa ambaye anahitaji sana kuombewa, huyo ni mimi. Na, kumbukeni, hudhurieni mkutano wa Ndugu Roberts wakati utakapokuja mjini, na mumpi salamu kutoka kwenye maskani.

⁴⁵ Kabla hatujasoma Maandiko, ni—ningependa tusimame kwa miguu yetu kwa dakika moja. Na, bila ya muziki, hebu na tuimbe tu pambio moja au mbili za wimbo huu mtukufu wa zamani wa kanisa, *Imani Yangu Inakutazamia Wewe*. Vema, kila mtu ajiunge moja kwa moja nami sasa, na hebu tuimbe. Na usifikirie jinsi unavyoimba, uimbe tu kwa utukufu wa Mungu. Utatuongoza katika huo, Ndugu Neville?

Imani yangu inakutazamia Wewe,
Ewe Mwana-kondoo wa Kalvari,
Mwokozi wa Kiungu;
Nisikie sasa ninapomba,
Ondolea mbali hatia yangu yote,
Ee unijalie tangu leo
Niwe Wako kabisa!

Nikitembea katika mzingile wa maisha yenye
giza,
Na huzuni imenizunguka,

Kuwa Kiongozi wangu;
 Amuru giza ligeuke kuwa mchana,
 Pangusa huzuni, hofu,
 Wala usiniache nikaondoka
 Karibu na Wewe.

⁴⁶ Huku vichwa vyetu vimeinamishwa, ningetaka kusoma maandiko matakatiifu ya Biblia, Mathayo Mt., mlango wa 7, kifungu cha 13 na 14. Na Bwana na aongeze baraka Zake nyingi tunapoyasoma.

Ingieni kwa kupitia mlango ulio mwembamba: maana mlango ni mpana, na njia ni pana iendayo katika maangamizo, nao ni wengi waingiao kwa mlango huo:

Bali mlango ni mwembamba, na njia imesonga iendayo uzimani, nao waionao ni wachache.

⁴⁷ Na tuombe. Ee Mungu, Wewe uliyemleta tena Bwana Yesu kutoka mautini na kutoka kaburini, na umemleta kwetu asubuhi hii kama Dhabihu iliyo hai, kwa unyenyekevu tunatoa maisha yetu Kwako upya, kwa mawazo kwamba Wewe utatujali sana sisi. Tulipokuwa tungali wenye dhambi, tumekufa katika dhambi na makosa, Wewe ulimtuma Mwana Wako wa pekee, aliyefanywa katika umbo la mwili wa dhambi, kuwa upatanisho kwa ajili ya dhambi zetu, kusudi yule Asiye na hatia, akiteseka kwa ajili ya walio na hatia, aweze kutupatanisha sisi pamoja Nawe.

⁴⁸ Na, Ee Mungu, kama kuna dhambi miongoni mwetu asubuhi hii, kitu ambacho kingeweza kumzuia Roho Mtakatifu asituletee Ujumbe wa Mungu kwa kila mmoja wa mioyo yetu, tunaomba kwamba, kwa unyenyekevu, Bwana, Wewe utusamehe makosa yetu. Tutakase kwa Damu ya Bwana Yesu. Ambao... Sisi tunajua, kwa nafsi zetu, sisi si kitu, na tunakiri kwamba sisi si kitu. Lakini Wewe ni mtakatifu, Wewe ni wa kweli, Wewe ndiye haki, Wewe ndiye Chemchemi ya rehema. Nasi kwa unyenyekevu tunajikokota hapo leo, kama nafsi zilizotubu. Kama ushuhuda ulivyotolewa hivi punde, kutoka Jamaica na kutoka Puerto Rico, na ambako Wewe umetenda kazi kuu namna hiyo, Ee Mungu, ni ishara ya kuja kwa yule Mwenye Haki.

⁴⁹ Jinsi Wewe ulivyomwokoia Ndugu Evans kutokana na meno ya sumu ya yule nyoka, kwa sababu yeye alikuwa mwaminio, na Maneno Yako sikuzote ni ya kweli. Sasa, Bwana, tuokoe na meno ya mauti asubuhi hii, pale ambapo adui ametuuma na kututia sumu. Jalia zeri Yako ya kuponya, asubuhi hii, Bwana, iloweshe kabisa roho zetu na kututakasa na uovu wetu wote. Ponya magonjwa ya miili ambayo imevunjwavunjwa na nguvu za adui. Wote walio katika Uwepo wa Kiungu, jalia waponywe.

⁵⁰ Nena nasi sasa kupitia Neno Lako lililoandikwa, Bwana. Nikiwa sijui la kusema, lakini Wewe utatupa hilo. Na Wewe utuonye, Bwana, na utufanye tayari kwa ajili ya Kuja Kwako.

Kwa kuwa tunaomba hili katika Jina la Yesu na kwa ajili Yake. Amina.

⁵¹ Sikuzote huwa nachelewa kidogo, kwa sababu nimengojea sasa. Na shule ya Jumapili, nadhani, imetoka. Lakini kuna kitu fulani kuhusu jambo hilo, wakati nijapo nyumbani hujisikia tu kama nina muda mwingi sana. Mnajua, tuna haraka kupita kiasi, kwa vyovyote vile. Kwa hiyo, tutamwamini tu Mungu.

⁵² Bwana wetu alikuwa akitoa onyo hili kali kwa watu wa kizazi Chake, watu ambao walikuwa wa kidini sana. Naye alisema, “Mlango ni mwembamba, na njia imesonga, iendayo Uzimani, nao watakaonia Hiyo ni wachache.” Sasa, haikuwa eti kwa sababu hawakuwa wa kidini. Walikuwa wa kidini sana. Na kwa sababu kwamba walikuwa wametumainia kanisa na katika kanuni fulani za kidini na madhehebu, na walikuwa wamemwamini (kwa kiasi) Mungu, walifikiria kila kitu kilikuwa sawa. Lakini Yeye alikuwa akiwaambia kwamba kutakuwa na wachache watakaolingia.

⁵³ Nami sijui asubuhi ya leo kama nisingeweza kufananisha kizazi hicho na kizazi hiki. Mnaona, ilikuwa ni mwishoni mwa majira ya Kiyahudi, na Yeye alikuwa anarejea nyuma kwa mambo mbalimbali na miisho mbalimbali ya majira mbalimbali, na alikuwa akiwaambia kwamba kitu kile kile ambacho kilifanywa katika majira yaliyopita kilikuwa kinafanywa mbele zao. Nao walikosa kukitambua. Na hebu tuone baadhi ya mambo ambayo Yeye alikuwa anayazungumzia.

⁵⁴ Wao, kwa mfano, hawangeweza kuamini kwamba Mungu alikuwa ndani ya Mtu yule. Hicho kilikuwa kizuizi kikubwa kuliko vyote ambacho iliwalazimu kukipanda, kilikuwa jinsi Yeye akiwa Mtu hata hivyo alijifanya Mwenyewe Mungu. Hawangeweza kuona jinsi Mungu angeweza kuishi katika mwili wa kibinadamu. Na katika nyakati zote, katika vipindi vyote, Mungu sikuzote ameishi ndani ya binadamu. Mwanadamu ni wakala wa Mungu. Katika kila kizazi, Mungu huzungumza na watu Wake kupitia midomo ya mwanadamu. Yeye sikuzote huchagua mtu fulani au kitu fulani ambacho Yeye anaweza kukitumia.

⁵⁵ Na Yeye aliwatajia, likiwa ni jambo la kukwaza, kuhusu Ibrahimu. Alisema, akawaambia, “Kama mnajiita wenyewe ‘wana wa Ibrahimu,’ Ibrahimu ‘baba’ yenu, aliiona siku Yangu naye alifurahi kuiona. Ibrahimu, nabii.” Na bila shaka Yesu alikuwa akiwakumbusha kwamba Yeye alikuwa amewahakikishia kuwa Yeye alikuwa Masihi, kwa sababu ishara ya Masihi ilikuwa inafuatana Naye. Na ilikuwa namna hiyo katika kila kizazi, hiyo, ishara ya Masihi. Lakini hata hivyo Yeye akijifanya Mwenyewe Mungu, Masihi Mwenyewe, hilo liliwakwaza. Hawangeweza kulielewa.

⁵⁶ Sasa, wakati Ibrahimu (ambaye walimwita baba yao) alipokutana na Mungu, Yeye alikuwa pia katika mwili, kwa sababu Yeye alikula nyama ya ndama, alikula ugali (na akanywa maziwa) na siagi, mbele ya Ibrahimu, na hata hivyo Yeye alikuwa Mungu. Ibrahimu alimtambua Huyo, Mungu, na kumwita “Elohimu,” ambaye ni Yehova Mwenyezi. Mtu aliyevaa nguo, na vumbi Mwilini Mwake, kisha akaketi chini ya mti, apate kivuli, na akala nyama na kunywa maziwa. Ndipo wale Wayahudi wenye haki, baridi, wenye mioyo katili, wenye ubinafsi, hawangeweza kumwamini Yeye kuwa Mwana wa Mungu, na walimwita Ibrahimu baba yao. Na Yeye alikuwa anawajulisha kwamba Yeye alikuwa anafanya mambo yale yale, katika mwili Wake, ambayo Mungu alifanya katika mwili mwingine wakati alipokutana na baba yao, Ibrahimu. Na Ibrahimu aliliamini jambo hilo. Na wao hawakuweza kuliadini.

⁵⁷ Unaona, wakati Ibrahimu alipokuwa ameketi chini ya hema lake kwa sababu alikuwa amekwishafanya chaguo, na chaguo hilo linaletwa mbele ya kila mtu ambaye amezaliwa katika ulimwengu huu. Mti wa mema na mabaya umewekwa mbele ya kila mtu. Na wakati Lutu, mpwa wake, na wachungaji wao walipoanza kubishania makonde; Ibrahimu, akiwa mtu mwenye haki, aliwaambia, “Na kusiwe na mabishano kati yetu. Ninyi chagueni tu njia mtakayokwenda.” Nafasi hiyo huja katika maisha ya kila mwaminio. Na iko mbele yako asubuhi ya leo, na iko mbele yangu.

⁵⁸ Lutu hakufikiria kwamba angerudi nyuma, lakini alianza kutazama kuelekea Sodoma ambako mambo yalikuwa rahisi. Na kuna mara nyingi ambapo huwa tunaangalia kuelekea njia iliyo rahisi. “Nitajiunga na hili kanisa fulani-fulani, na, unaona, hakuna mtu atakayesema chochote dhidi yake, kwa sababu ndilo kanisa lililo kubwa kuliko yote katika jiji hili.” Njia iliyo rahisi! Mara nyingi tunafanya hivyo, ambapo, tumekosea!

⁵⁹ Kumbuka, kama ukimfuata Kristo, utachukiwa na watu, kwa kuwa wote wale ambao wanaishi maisha ya utauwa katika Kristo Yesu watapatwa na mateso. Na kama ukija kwa Kristo, hutakuja kwa njia ya kanisa lolote au dhehebu lolote, au kanuni yoyote ya imani. Utakuja kwa Damu, hiyo ndiyo njia pekee ya kuingia. Na huwezi kuja na mtu yeyote, utakuja peke yako na kusimama katika maungamo yako mwenyewe na imani yako mwenyewe. Hutaingia ndani kwa njia ya mchungaji, au kwa imani ya mama yako. Utakuja kama mtu binafsi utakapokuja kwa Mungu! Na mara nyingi tunafanya hizo chaguo za kipumbavu.

⁶⁰ Vipi kama Lutu, wakati alipoona kila kitu rahisi. . . ? Aliona mahali ambapo palikuwa na fedha nyingi na umaarufu mkubwa, kwa sababu angekuwa mgeni, na mtu mwerevu, mwenye elimu, mwenye saikolojia nyingi, na angeweza kufanya mambo fulani na bado ashikilie dini yake. Aliwazia, “Nina imani kwa Mungu,

kwa hiyo nitakwenda tu chini huko Sodom na ni—nitapata fedha zaidi, nami nitakuwa mtu mashuhuri, labda mhubiri wa ajabu.” Unaona, una chaguo la kufanya.

⁶¹ Na washiriki wanalo chaguo la kufanya. “Nitakwenda kwenye hili kanisa fulani kule. Loo, kila mtu mjini hufikiria hili lazidi yote! Naam, meya wa jiji ni wa kanisa hili.” Sasa, angeweza kuwa ni wa kanisa ambalo lilikuwa zuri sana, lakini bado inakupasa kulipima kanisa hilo na watu wake kwa Maandiko. Wakati mwingine wao huenda kwa sababu ni njia inayopendwa na watu, wa—watu huvalia vizuri zaidi ambao huenda mahali fulani. Basi hapo ndipo tufanyapo ko—kosa baya sana. Sasa angalia hili.

⁶² Naye Ibrahimu, kitu pekee alichoweza kufanya kilikuwa ni kuchukua chaguo la pili. Na wakati mwingine chaguo la pili ni zuri kuliko la kwanza, kama likichukuliwa namna hiyo. Angalia, haikuwa muda mrefu, wakati Lutu alipoona jiji lile kubwa, hakumwona mkewe akigeuka kuwa nguzo ya chumvi, hata hivyo, hakuona moto ukiliteketeza hilo jiji. Lakini Ibrahimu alifuata njia ya wachache wa Bwana waliodharauliwa. Alikaa jangwani.

⁶³ Na, hata hivyo, vipi kama Sara angalisema...Sasa kumbuka, Sara alikuwa mwanamke aliye na sura nzuri kuliko wote nchini kote. Hakukuwa na mwanamke mwenye sura nzuri kama Sara. Kila mmoja, aliyemwona, alimpenda. Sasa, ingelikuwa rahisi jinsi gani kwa Sara kuchukua chaguo la aina hiyo. Lakini alichagua kukaa na Ibrahimu.

⁶⁴ Loo, enyi wanawake, usimwache ibilisi akupofushe, kuwa maarufu na kujiunga na *hili* na *lile*. Wewe dumu na Kristo! Kwa maana, saa imekaribia, maangamizi makuu yako mbele, mabaya kuliko Sodom na Gomora, kwa nchi hii. Sodom na Gomora itakuwa na sifa njema kuliko nchi hii.

⁶⁵ Sasa, wakati Ibrahimu alipokuwa amefuata njia ile ambayo alipewa na Mungu, naye alikuwa na nchi kame, hakufanikiwa kamwe. Lakini hata hivyo alijua kitu kimoja, alimtumikia Mungu na alimwamini Mungu.

⁶⁶ Kwa hiyo siku moja walikuja watu watatu, nao walikuwa wamejaa vumbi na wamechoka, na Ibrahimu akawahurumia, akasema, “Njoni mketi chini ya mwaloni kwa muda kidogo tu.” Na wakati alipokuwa amesimama pale akizungumza nao, alitambua kwamba hawakuwa tu watu wa kawaida, kwa mazungumzo yao. Walikuwa tofauti. Kisha Ibrahimu akaenda akachinja ndama na akaagiza aandaliwe, kisha akamwagiza Sara atengeneze mikate na awe tayari kuwapa chakula.

⁶⁷ Sasa kumbuka, wawili kati yao walikuwa Malaika, Malaika katika mwili wa kibinadamu, na mmoja wao alikuwa Mungu Mwenyewe. Na yule Mmoja ambaye alikuwa Mungu alikuwa ameelekeza mgongo Wake kwenye hema.

⁶⁸ Basi Sara alikaa hemani. Napenda kuona mwanamke akikaa mahali pake namna hiyo, si kutoka nje na kumwambia mumewe la kufanya, na kila wakati mtu fulani ajapo. Lakini alikaa hemani. Hapana shaka, labda akisafisha vyombo au akifanya kitu fulani.

⁶⁹ Na huyu Mmoja ambaye alikuwa Mungu, Yeye alikaza kuangalia huku na huko kuelekea Sodoma, Naye akawaambia atakalotenda. Basi Malaika wawili walikwenda huko kuhubiri Injili. Lakini Mmoja alibaki nyuma, huyo Ndiye aliyekuwa Mungu, Naye akasema, “Sitamficha Ibrahimu siri ambazo nazijua, kwa sababu yeye atakuwa mrithi wa ulimwengu.”

⁷⁰ Loo, tuna haki asubuhi ya leo, kanisa, kujua siri za Kuja kwa Bwana. Kwa kuwa, “Heri wapatanishi, wataitwa watoto wa Mungu. Heri wenye njaa na kiu, watashibishwa. Heri wenye moyo safi, maana hao watamwona Mungu. Heri wenye upole, maana hao watairithi nchi.” Basi, kama kanisa la Mungu aliye hai litairithi nchi, hakuna siri linayofichwa.

⁷¹ “Yote Baba aliyoniambia Mimi, nimewaambia,” alisema Yesu. Nao hawangeweza kumwamini Yeye.

⁷² Kwa hiyo katika siku za Ibrahimu, kama Yeye alivyokuwa anawakumbusha, alisema kwamba wakati Ibrahimu alipokuwa anazungumza na Malaika, na mgongo Wake umeelekezwa kwenye hema, Naye akamwambia Ibrahimu atamzuru na mtoto. Naye Sara, akiwa ndani ya hema, alicheka. Ndipo Yeye akasema, “Kwa nini Sara akacheka?” Je, alikuwa anaonyesha nini? “Kwa nini Sara akacheka?” Ilikuwa saa chache tu kabla ya maangamizi, wakati jambo hilo lilipotukia. Kabla tu ya maangamizi, huo moto ulishuka kutoka mbinguni na kulitekeza lile jiji, na ishara hiyo ikatendeka.

⁷³ Naye Yesu akasema, “Mwapotea,” kwa wale madaktari mashuhuri wa uungu, kwa taifa la kidini mahali ambapo mamilionini halisi walikuwa waaminio. Yeye alisema, “Mwapotea, kwa kuwa hamyajui Maandiko wala Uwezo wa Mungu.” Kwa kizazi kama hicho, ambacho kilikuwa cha watu waliofundishwa vyema, watu waliokuwa wasomi na waliotelewa kanisani. Mtoto alipozaliwa, alikuwa mali ya kanisa. Ilibidi uwe Mwisraeli. Siku nane baada ya kuzaliwa kwako, ilikuwa kutahiriwa, nawe ulikuwa Mwisraeli kwa kuanzia. Na ukuhani ulitoka kwa Walawi, ambao walifunzwa kwa mamia ya miaka katika Maandiko. Hata hivyo Yesu alisema, “Mwapotea, kwa kuwa hamyajui Maandiko!” Waliyajua katika kitabu chao wenyewe cha kujifunzia, waliyajua kwa katekismo zao, waliyajua kwa theolojia yao wenyewe. Lakini Yesu alisema, “Hamyajui, Maandiko, wala hamjui Uwezo wa Mungu. Kama mngalimjua Ibrahimu, mngenijua Mimi. Kama mngalikuwa watoto wa Ibrahimu, mngenijua Mimi, kwa sababu Ibrahimu alishangilia alipoiona siku Yangu, kwa maana alitangulia kuiona siku hiyo.

Wakati niliposimama mbele yake huko nyuma, katika mwili wa nyama, na nikafanya jambo hili, alijua ilikuwa Mimi, naye aliniita Mimi ‘Elohimu.’ Lakini hapa ninatenda jambo lile lile mbele yenu, nanyi mwaniita Mimi ‘Beelzebuli.’”

“Loo,” wangesema, “tunaye Ibrahimu baba yetu”.

“Kumwita Ibrahimu ‘baba’ yenu?”

⁷⁴ Alisema, “Mbona, sisi, tu washiriki wa kanisa. Sisi ni taifa la kidini. Sisi ni watu mashuhuri. Tu watu wa Mungu!”

Yesu akasema, “Ninyi ni ibilisi, ndiye baba yenu.”

⁷⁵ Ninaweza kukifananisha kizazi hicho na kizazi hiki, leo hii, wakati ambapo kuna mamilioni halisi ya watu ambao hukiri Ukristo, na hawajui zaidi kuhusu Mungu kuliko Mhotentoti awezavyo kujua kuhusu hekaya za Kimisri. Kuna wanaume na wanawake leo hii, mamilioni hasa wanaokiri kuwa Wakristo ambao humtaja Kristo, wasiojua kanuni ya kwanza ya Nguvu za kufufuka Kwake, na hawajawahi kuonja wema Wake. Hawajawahi kuguswa na Nguvu Zake. Macho yao yamepofushwa wasiione Kweli.

⁷⁶ Kasema, “Ninyi ni vipofu, viongozi wa vipofu. Si . . . ninii . . . kipofu akimwongoza kipofu, si wote watatumbukia shimoni?”

⁷⁷ Basi waliwazia, “Sisi ni Wakristo. Sisi ni waaminio. Tu washiriki wa makanisa ya juu zaidi ya yote yaliyopo. Marabi wetu ni wasomi waliofunzwa vizuri kuliko wote waliopo.” Na hata hivyo Yesu aliwaambia hata hawakuyajua Maandiko.

⁷⁸ Unaona jinsi Mungu alivyoyaficha kwa wenye hekima na akili, na kuwafunulia watoto wachanga ambao watajifunza? Loo, Nguvu kuu na kutokuwa na kikomo kwa Mungu! Jinsi Yeye alivyo mwema kwa wale wenye hamu ya kuenenda kwa unyofu mbele Zake! Hatawanyima chochote chema.

⁷⁹ Na kuona siku ambayo taifa letu, ulimwengu wetu, umepotoka kwa jambo lile lile!

⁸⁰ Yesu alitaka kuwasahihisha vizuri. Walisema, “Loo, Ibrahimu ni baba yetu. Nasi tutakuwa Utukufuni, usijisumbue na jambo hilo, kwa sababu tunamwamini Mungu. Sisi ni maprofesa, na tunamwamini Mungu, na tunawafundisha watu wetu. Basi Wewe ni nani unayekuja hapa na ma—maskini ishara ya kale ya ajabujabu na kujaribu kusema eti ni Mungu? Wewe si kitu ila Beelzebuli.” Haya basi, walikuwa na kanuni zao za imani na madhehebu yao.

Yesu aliwaambia, “Ninyi ni ibilisi.” Wazia hilo!

⁸¹ Nami ninge kifananisha kizazi hicho na hiki, siku hizi wakati ambapo tunao mamilioni wanaojiunga na makanisa, tuna makumi ya maelfu. Na Mungu anashuka kuja kuishi ndani ya kanisa Lake tena, na kutenda mambo yale yale ambayo Yeye alitenda kule, ili kujifanya Mwenyewe kuwa yeye yule jana, leo,

na hata milele. Na watu wanalipa kisogo, kila mara, baadhi yao ili kuwa maarufu, wengine kuepuka kufanya chaguo. Jambo hili linalazimishiwa watu! Yakubidi kufanya chaguo. Huwezi kuwa asiyePENDelea upande wowote. Yakubidi kusema “ndiyo” au “la.” Hutatoka nje ya huo mlango ukiwa mtu yule yule jinsi ulivyoingia. Huwezi kufanya hivyo. Unalo chaguo la kufanya. Lifanye kwa ajili ya Kristo asubuhi ya leo.

⁸² Walifikiri kila kitu ambacho ni cha kanisa kingeokolewa. Yesu alisema, “Mlango ni mwembamba, na njia imesonga, nao watakaona ni wachache.”

⁸³ Hebu niwaonye asubuhi hii, kanisa, iweni waangalifu. Inachukua muda siku hizi, katika kizazi chetu kinachojihesabia haki na kinachojitegemea cha unafiki ambacho tunaishi ndani yake. Saa ambayo wanaume na wanawake wanasimama makanisani na kwenye viti vya kanisa na kuimba nyimbo za kumtukuza Mungu, na kutoka nje ya kanisa hilo na kuvuta sigara, na kunywa wiski, na kwenda kwenye dansi, na—na kuishi kwa mambo ya ulimwengu, na kutoa mizaha michafu, ya lugha chafu, na kujiita “Wakristo.” Wakati wanaume na wanawake wanaweza kutoka kwenye mimbara au kutoka kanisani, na kutoka mahali pa Nguvu za ufufuo, ambapo ishara ile ile ya Masihi inatenda kazi miongoni mwao, na wasiwe kiumbe kipya katika Kristo, kuna kasoro. Wakati magazeti yanaweza kuitangaza kwa uvumi mkubwa; na kutoka pwani hadi pwani, huku na huko, kutoka pande za nchi za Kaskazini zenye barafu mpaka kwenye misitu ya tropiki ya Kusini, Mungu huituma, na watu kila mara wanaipa kisogo. Basi tuseme nini, tufanye nini? Tunarejea kwenye Maandiko ambako Yeye alisema, “Mlango ni mwembamba, na njia imesonga, nao watakaona ni wachache.”

⁸⁴ Yeye alisema, “Kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu, ndivyo itakavyokuwa katika kuja Kwake Mwana wa Adamu.” Sikilizeni, katika siku za Nuhu, ulimwengu ulikuwa umejawa na watu kama ulivyo leo. Sayansi yao ilikuwa inazidi yetu. Walijenga masfiniksi na mapiramidi na kufanya mambo ambayo hatuwezi kufanya leo. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] Watu werevu sana, sana. Basi kumbuka, sayansi inasema leo, “Ni dakika moja kabla ya usiku wa manane.” Ni dakika moja kabla ya saa kugonga usiku wa manane. Muda umekwenda sana kuliko tunavyodhanja. Natumaini kwamba—natumaini kwamba Roho Mtakatifu atalizamisha hili katika kila moyo wa mwaminio, “kama siku za Nuhu”!

⁸⁵ Wangapi waliokoka katika siku za Nuhu, kutoka katika kizazi hicho? Wanane, wanane kutoka katika mamilioni mengi. Yeye alisema, “Ndivyo itakavyokuwa katika Kuja kwake Mwana wa Adamu.”

⁸⁶ “Na kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa katika Kuja kwake Mwana wa Adamu.” Katika makumi ya maelfu, kulikuwa na watatu waliookolewa.

⁸⁷ Ungeniambia basi, “Mhubiri, vipi kuhusu wale maelfu wote ambao watakuja pamoja Naye?” Sasa, ndugu, hao wametoka katika vizazi vingi.

⁸⁸ Nitashangaa kama watu dazeni moja watatoka katika kizazi hiki. “Mlango ni mwembamba, na njia imesonga, nao watakaona ni wachache.”

⁸⁹ Loo, najua makanisa, kile wasemacho, “Kama ukiweka jina lako katika kitabu na unakuwa mshirika, *hiki*, uko sawa.” Hakuna Andiko kama hilo. Kama kila kitu kimeandikwa jina lake kwenye kitabu, na katika—katika kanisa, kutakuwa mabilioni mara mabilioni mara mabilioni, kila kitu kitaingia. Basi aina zote za roho zitakuweko mle, basi Mbinguni kutakuwa na hali ya aina gani? Wazia hilo sasa.

⁹⁰ Mtu fulani angeniambia, “Sasa ngoja kidogo, Ndugu Branham. *Fulani-na-fulani*, nimewasikia wakinena kwa lugha, najua wataingia.”

⁹¹ Hilo halimaanishi wataingia hata kidogo. Paulo alisema, katika Wakorintho wa Kwanza 13, “Nijaponena kwa lugha za wanadamu na malaika, kama sina upendo, si kitu mimi.”

⁹² “Loo, nilienda kwenye mkutano wa *Fulani-wa-fulani*. Loo alifanya kazi kubwa mno. Nilimwona akiwafanya vipofu kuona.”

⁹³ Bado angeweza kupotea. “Wengi watakuja Kwangu siku hiyo na kusema, ‘Bwana, sikuhubiri kwa Jina Lako, nikatabiri? Si, katika Jina Lako, nimetoa pepo wachafu? Si, katika Jina Lako, nimefanya kazi nyingi kubwa?’ Yeye atasema, ‘Ondokeni Kwangu, ninyi mtendao maovu, hata sikuwajua ninyi.’” “Mlango ni mwembamba, na njia imesonga, nao watakaona ni wachache.”

⁹⁴ Hebu niwape maoni yangu yatakayowashtua. Kulingana na sayansi ya tiba, katika jiji la Chicago, kulingana na takwimu za daktari, kuna visa vya kutoa mimba elfu thelathini katika Chicago peke yake, katika muda wa siku thelathini, walivyo navyo madaktari. Ni maskini vidonge hivi vingapi na kadhalika wanavyomeza, ambavyo ni visa vya kutoa mimba?

⁹⁵ Takwimu zinaonyesha, katika Marekani, kwamba kuna watoto wa haramu wengi zaidi wanaozaliwa kuliko watoto wa ndoa takatifu. Hivi ulijua Biblia ilisema, katika Kumbukumbu la Torati 14:2, kwamba “mtoto haramu, ingechukua miaka mia nne kwa uzao huo kuisha”? Watoto wa watoto wa watoto wa watoto wa watoto wao hawawezi kusimama katika kusanyiko la Bwana, miaka mia nne, vizazi kumi. Miaka arobaini kwa kizazi. Babu wa babu wa babu wa babu wa babu wa babu wa babu

yao alikuwa mtoto haramu, hatambuliwi! Sasa nini? Nionyeshe mahali ambapo ilibadilishwa.

⁹⁶ Tunafikia nini? Na sasa watoto haramu, kwa sababu ya uzinzi, na wanawake wenye dhambi wakivalia barabarani kama wanaume, ambalo ni chukizo machoni pa Mungu, wavuta sigara, wanywaji pombe kali ya mchanganyiko, wanaodai eti ni Wakristo. Mungu na aepushe kundi kama hilo la makahaba! Hiyo ni kweli. Halafu wanajiita Wakristo? Si ajabu Yesu alisema, “Mlango ni mwembamba, na njia imesonga, bali watakaonia watakuwa wachache.”

⁹⁷ Hawatajinyenyekeza. Ni wagumu. Angalia, wakati Daudi alipoambiwa kuhusu dhambi yake aliyoifanya, upesi alitubu, ndipo Mungu akampenda kwa jambo hilo. Ukiwaambia kuhusu dhambi zao, watasema, “Sitaingia mlango huo tena.” Kwa nini? Wana mahali pengi pa kwenda, wanaweza kwenda kwenye matundu hayo haramu ambayo yatavumiliana na hayo. Lakini wakati umewadia ambapo yabidi wahubiri wavae silaha zote za Mungu na kuhubiri Neno pasipo kupatana, Injili. Watu wanapaswa kujinyenyekeza.

⁹⁸ Hakuna uaminifu miongoni mwa Wakristo tena. Wanataka waseme, “Mimi ni Mmethodisti, mimi ni Mbaptisti, mimi ni Mpentekoste,” hiyo haimaanishi *hilo* kwa Mungu. [Ndugu Branham anadata kidole chake—Mh.]

⁹⁹ “Nilinena kwa lugha, nilifanya miujiza.” Tunatilia mkazo wote katika jambo hilo, wakati ambapo hilo ni mojawapo ya mambo yanayopofusha sana ambayo wangeweza kufanya. Hakika. Mvua huwanyeshea wenye haki sawasawa na wasio haki. Mvua hunywesha mazao vile vile kama inavyoyanywesha magugu, Roy. Mvua ile ile, Roho Mtakatifu yeye yule huwashukia watu. Hilo bado halimaanishi. . . . Asili yao haina budi kuwa tofauti, kutoka ndani hadi nje. Siyo dhihirisho la nje au onyesho, lakini Roho wa ndani wa Mungu aliye hai ambaye humfanya mtu huyo kiumbe kipya, anayenyenyekeza moyo wa mwanamume au mwanamke huyo mbele za Mungu.

¹⁰⁰ Unasema, “Mhubiri, wataka kuniambia unatilia shaka dazani moja kutoka katika haya mamilioni na watu bilioni nne ulimwenguni?” Nina shaka kama kuna dazani moja ambao wataingia katika Unyakuo. Wazia hilo! Ninawaambia kile Yesu alichosema hapa katika Injili. Wazia hilo!

¹⁰¹ Imefikia wapi? Kwa sababu uzinzi uliingia miongoni mwa watu, watoto wa haramu walianza kuzaliwa, hilo huwafutilia mbali. Unaona, tungeweza kusimama hapa kwa saa kadha, tukiweka mambo hayo, na unaweza kuona kwamba tunaishi katika kizazi cha watu kilichopotoka, kilicholaaniwa, kizazi kilichooza kabisa. Si ajabu hawawezi kuona ishara, si ajabu hawataisikia Injili, wamekuwa wagumu, hata hivyo ni wa kidini na waadilifu.

102 Hivi Yesu hakusema kwamba, “Roho anena waziwazi, katika siku za mwisho watakuwa wakaidi, wenye kujivuna, wapendao anasa kuliko kumpenda Mungu, wasiotaka kufanya suluhu, wasiojizua, wakali, na wasiopenda walio wema, wenye mfano wa utauwa”? Unaona? Loo, unaweza ukapaza sauti, hakika. Unaweza kunena kwa lugha, hakika. Imani itatoa pepo, hakika. Lakini hilo silo tunalozungumzia.

103 Basi ungeniambia, “Ndugu Branham, alama ya Mkristo ni ipi? Ni nani atakayeokoka? Utaokoka, Ndugu Branham?” Ninatumainisha hilo kwa Mungu. Sijui. Ninaamini kwamba nimeokoka. Ninalinganisha maisha yangu, kila siku, na Neno. Kama hayaambatani na Neno hili, basi kuna kasoro, yanibidi nirudi nyuma na kujisahihisha.

104 “Vema,” unasema, “Ndugu Branham, wakati watu wanaponena kwa lugha, hilo halimaanishi wameokoka?” La, bwana! La, hash! Nimewasikia wachawi na walozi wakinena kwa lugha, kila aina ya upuuzi. Nimeona watu wakinena kwa lugha na kuishi na mke wa mtu mwingine. Nimeona watu wakinena kwa lugha, na kurukaruka juu chini na kupaza sauti kana kwamba nyumba inaungua moto, na kushika njia kwenda kufanya magendo, na kuiba, kusema uongo, na kila kitu. Unaweza je kutazamia jambo hilo? La, bwana.

105 Washirika wa kanisa, mashemasi kanisani, watawa iwezekanavyo. Naam, unafikiri wangenunua petroli Jumapili? La. Lakini Jumatatu wanafanya kitu ambacho ni kichafu na kilichooza na cha kutia aibu. Mungu hukaa ndani ya moyo, sio nje, ni kitu kinachokuja kutoka moyoni.

106 “Mlango ni mwembamba, na njia imesonga, nao watakaoiona ni wachache.” Kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu, wanane kutoka katika hayo mamilioni; kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, watatu kutoka katika mamilioni; ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwake Mwana wa Adamu.

107 Na unauona uharibifu tuliomo. Unaona jinsi ambavyo kila wazo, binadamu, yeye hutoka nje huko na Ibilisi huwafanya wahubiri stadi wasimame mimbarani na kupita nayo.

108 Hivi majuzi mtu mmoja alisema, “Singeuruhusu katika mimbara yangu, ungewafanya wanawake wangu wapate kichaa.” La, tayari wako hivyo. Ingewarudisha kwenye akili zao timamu, kuwaambia hapo waache kuvaa nguo hizi na kadhalika. Basi, vema, mtu fulani hana budi kutenda jambo hilo.

109 Nilimwambia mke wangu, “Je, nina kichaa, mimi mwenyewe? Nimerukwa na akili? Au, nina nini?” Kitu fulani mle ndani hakiwezi kutulia. Yanibidi niliseme, sijali mtu yeyote anasema nini.

110 Kasema, “Utaharibu huduma yako.” Vema, huduma yoyote ambayo Injili itaharibu, yapaswa kuharibiwa.

Mungu atupe ujasiri kusimama kwa ajili ya Kweli na kusema Kweli juu yake! Hiyo ni dhambi, aibu!

¹¹¹ “Mlango ni mwembamba,” alisema Yesu, “na njia imesonga.” Na ninyi ambao mnafikiria mamilioni, na ninyi nyote Wamethodisti, Wabatisti, Mpresbiteri, Wapentekoste mnaoingia, mtapumbazwa siku hiyo. Yesu alisema, “Wengi watakuja na kuketi katika Ufalme, waseme ‘Nina haki ya kuwa hapa.’” Yeye alisema, “Lakini wana wa Ufalme watawatupilia nje. Kutakuwa na kulia na kuomboleza na kusaga meno.” Ni afadhali ujichunguze asubuhi ya leo, ewe Mkristo. Kutakuwa na kumi mara mamilioni mara mabilioni ya wanaokiri kuwa Wakristo, na walio waaminifu sana katika maisha yao, ambao wataukosa huo mlango. Yesu alisema hivyo.

“Ni wangapi wanaingia?”

¹¹² Sijui ni wangapi watakaoingia. Jambo tu ni kwamba, “Mungu, nijalie niwe mmoja wao!” Jambo ndilo hilo. Yeye ndiye Hakimu. “Nijalie kuwa mmoja.”

¹¹³ Unasema, “Ndugu Branham, unawezaje kujua basi unapokuwa Mkristo?”

¹¹⁴ Sijui. Lakini hebu nikwambie Andiko linavyosema. Hakika unaamini Hilo. Roho Mtakatifu alipotumwa duniani, Mungu alinena kupitia kwa Roho Mtakatifu. Alimtuma malaika mbele—mbele, kwanza. Naye akasema, “Pita kati ya mji na miongoni mwa watu, ukawatie alama katika vipaji vya nyuso zao, wale ambao wanaugua na kulia kwa sababu ya machukizo, wakisahihisha mambo hayo.”

¹¹⁵ Chukizo ni nini? Mwanamke ambaye atavaa vazi limpasalo mwanamume. Inamfanya Mungu achefuke. Uliwahi kufika mahali ambapo kuna jambo la kuchukiza? Jinsi jambo hilo linavyokuchefua! Huwezi kulivumilia. Mwanamke ambaye atavaa vazi limpasalo mwanamume, hivyo ndivyo linavyomfanya Mungu ajisikie; waweza uimbe kwenye kwaya, waweza uombe kila siku, na kupaza sauti kila siku, au umwishie Mungu kila siku, Mbele za Mungu umehukumiwa. Hivyo ndivyo Maandiko yasemavyo hasa. “Chukizo!” Nao wale ambao wanashikilia hayo watakuwa na sehemu katika mambo hayo.

¹¹⁶ Mungu tupe neema kupinga mambo hayo. Kama inakubidi kusimama peke yako, simama hapo na ushikilie Neno la Mungu mkononi mwako. Halitashindwa kamwe.

¹¹⁷ Sasa tumefikia siku, ambapo, machukizo ya watu. Na Malaika ametoka kwenda akitia muhuri tena. Nitafutie mtu mmoja Jeffersonville, kama unataka kujua ni nani atakayeingia, nitafutie mtu mmoja katika mji wetu ambaye huugua na kulia, kila wakati akiudhiwa na kuchoshwa, na akiomba kwa sababu ya machukizo yanayofanyika jijini. Waweza kuinua mkono wako na kuuweka juu ya mtu mmoja? Basi chukua Andiko hili, “Mlango ni mwembamba, na njia imesonga, iendayo Uzimani,

nao waionao ni wachache.” Hao ndio pekee ambao walikuwa watiwe muhuri.

¹¹⁸ Loo, naweza kukuonyesha wengi wanaokwenda kanisani. Naweza kukuonyesha wengi waimbao kwenye kwaya. Naweza kukuonyesha wengi wafundishao shule ya Jumapili. Naweza kukuonyesha wengi ambao ni wakuu wa—wa mashirika mashuhuri. Naweza kukuonyesha wengi wanaopaza sauti, wengi wanaonena kwa lugha, wengi wanaoshughulika katika kazi ya Injili.

¹¹⁹ Lakini nionyeshe mmoja ambaye katika kilindi cha moyo wake anasumbuka mno kwa sababu ya dhambi za ulimwengu! Nionyeshe mhubiri ambaye atasimama na kuhukumu hayo madhehebu. Nionyeshe mhubiri ambaye atasimama leo na kusema mambo hayo, na kuyahukumu hayo madhehebu. Afadhali asiyahukumu, atafukuzwa, hiyo ndiyo tikiti yake ya posho.

¹²⁰ Si ajabu Billy Graham alimwambia Jack Moore, alisema, haoni vipi mikutano yangu inavyosimama, akasema, “Yeye si Mbaptisti, wala yeye si Mmethodisti au Mpentekoste.” Kasema, “Na wote hao wanampinga.” Hakika, sisemi kwamba . . . Sababu niliyosema, siwezi kuisema nje hadharani. Naisema kwa kanisa langu mwenyewe. Ninayo mapambano, kwa sababu saa ya kujaribiwa imenijilia.

¹²¹ Wao husema, “Kama utakuja, itakuwa sawa, lakini usiseme lolote kuhusu Hilo.” Afadhali basi usiseme lolote.

¹²² Nitahubiri ambalo Mungu amesema hubiri! Hiyo ni kweli. Mmoja wa hao wanane atakuwa mahali fulani. Mmoja wao atakuwa mahali fulani. Lakini siku ile sitaki kuwa na hatia ya kusema nilipatana kwa sababu ya kanuni fulani ya imani au fundisho fulani la kanisa, au madhehebu fulani. Nimehubiri Kweli!

¹²³ Wao husema, “Kwa nini wewe, kwa nini huduma yako, Ndugu Branham, ambayo inaonekana kuwa kubwa mno, kwa nini isisambae kama wafanyavyo watu hawa wengine?”

¹²⁴ Jambo ndilo hilo papo hapo. Ndilo hilo. Naenda katika jiji, unafikiri Assemblies of God watashirikiana nami? Si kwa yale ninayoamini, hawashirikiani. Naweza pengine nimpate mmoja mara moja moja. Unafikiri Wamethodisti wangeshirikiana? Jaribu, uone. Hebu uwe meneja wangu kwa juma moja. Kama ukienda humo, utakwenda katika Jina la Yesu. Hiyo ni kweli.

¹²⁵ Loo, bila shaka, wanakupeleka kule, hakika, wanakupeleka kule mahali fulani, na ili usihusike nao kwa namna zozote namna hiyo. Na ndipo wakati unapoondoka, wanasema, “Loo, sasa, Ndugu Branham amechanganyikiwa kidogo tu akilini, mwajua. Yeye . . .”

126 Kama nimechanganyikiwa akilini, basi Biblia imekosea katika Mafundisho. Hivyo ndivyo Biblia ilivyosema! Ndiyo, bwana. Angalia!

127 Yesu alisema, “Kwa nini mnaniita ‘Beelzebuli’? Mlimwamini Sulemani, ishara yake ya upambanuzi. Mliamini siku yake. Malkia wa Kusini alikuja kutoka pande za mwisho za dunia, kuona kipawa kile, naye alikiamini alipokiona. Nanyi mnakaa na kukiangalia kila siku, na hamkiamini.”

128 Na ndugu Zake Mwenyewe hawakumwamini Yeye. Kasema, “Mnapanda kwenda kwenye karamu,” Yeye akasema, “lakini Mimi siendi sasa.” Yeye alienda njia nyingine, kwa sababu ndugu Zake Mwenyewe hawakumwamini Yeye. Hiyo ni kweli. “Mlango ni mwembamba, na njia imesonga, nao watakaiona ni wachache.”

129 Wakati ilipofika kwa wanafunzi, kwenye shindano la kuamua, walikuwa wapi? Mwanamke na mwanamume walisimama msalabani pamoja Naye, Yohana na Mariamu. Hao wengine walikuwa wamekwenda zao.

130 Hili ndilo shindano la kuamua. Huu ndio wakati. Huu ndio wakati ambao Mungu anafanya mambo. Huu ndio wakati ambapo Masihi yupo duniani. Huu ndio wakati ambapo Nguvu za Mungu zinatenda kazi ndani ya watu Wake. Nao wanawaita “watakatifu wanaojifingirisha, wenye kichaa, wendawazimu,” loo, mambo kama hayo. Lakini saa imewadia!

131 Hakika kutakuwa na masikitiko makubwa kwenye hukumu.

132 Loo, muuza pombe haramu, anajua mahali atakapokuwa kwenye hukumu. Vivyo hivyo shabiki wa pombe anajua atakuwa wapi. Kadhalika kahaba anajua atakaposimama. Kadhalika mcheza kamari anajua mahali atakaposimama. Kadhalika mlevi anajua mahali atakaposimama. Hatasikitishwa.

133 Lakini mahali kusikitishwa kutakapokuwa, ni wale waliodhania walikuwa sawa. Hapo ndipo penye sikitiko. “Walipofika kule, walisema, ‘Hakika, tulitoa pepo katika Jina Lako. Sisi ni wahubiri. Tu washiriki wa makanisa fulani-fulani. Tulitenda miujiza mikuu. Loo, tulihubiri! Mbona, nimekuwa—nimekuwa mtumishi kanisani. Nimekuwa askofu. Nimekuwa *hiki*.’ Ondokeni Kwangu, enyi mtendao maovu, sikuwajua kamwe.” Haya basi. Huko ndiko kusikitika. Alisema, “Watoto wa watoto wao watakuja na kuketi katika Ufalme, waseme, ‘Tunayo haki ya kuwepo hapa,’ nao watatupwa katika giza la nje ambako kutakuwa na kulia na kuomboleza na kusaga meno.” “Mlango ni mwembamba, njia imesonga, iendayo Uzimani, watakaoina ni wachache.”

134 Kwenu ninyi, watu wangu wapendwa, asubuhi hii, sikilizeni hili. Sikulitunga hili. Ninawajibika kulisema. Hilo tu ndilo ninalowajibikia. Kama sitahubiri mahubiri mengine katika maisha yangu, huo ni Ukweli: kutakuwa na watu wachache tu

watakaokolewa. Kumbuka tu hilo: wachache sana. Hebu uwe mmoja wao.

¹³⁵ “Hao ni akina nani, Ndugu Branham?” Sijui. Hakuna mwingine ajuaye. Tunautimiza wokovu wetu wenyewe kwa hofu na kutetemeka.

¹³⁶ Lakini wewe jilainishe na Mungu. Kama moyo wako hauendi sawa na hiyo Biblia, basi kuna kasoro, kuna kasoro. Haidhuru kanisa lako linasema nini, huwezi kuingia kwa hilo. Yakubidi uingie kwa lile ambalo Mungu alisema. Hiki ndicho Kitabu utakachohukumiwa kwacho, Biblia. Dumu Nacho!

¹³⁷ “Loo,” unasema, “vema, nimebatizwa katika Jina la Bwana Yesu.” Hiyo ni sawa, hiyo ni Biblia. Lakini kama maisha hayo hayaambatani nayo, haikukufaidi sana kubatizwa.

¹³⁸ Unasema, “Vema, nimempokea Roho Mtakatifu.” Hilo ni jema, hilo ndilo lililokupasa kutenda. Lakini kama maisha hayamo mle ndani!

¹³⁹ Kumbuka, gugu hupokea nguvu ile ile ambayo huiangukia ngano kuifanya ikue, hulifanya gugu lipaze sauti, pia. Maskini gugu dogo lililokomaa linasimama moja kwa moja na kufurahi tu kama vile ngano inavyofurahi. Hiyo ni kweli, huishi kwa uhai ule ule. Na mwenye dhambi anaweza kukaa katika Uwepo wa Mungu, apige vifijo vya ushindi, na kuishi kama Mkristo. Lakini kama hakuna kitu tofauti moyoni! Angeweza kuwa na Nguvu zile zile za kutoa pepo wachafu. Yesu alisema hivyo. Anaweza kuhubiri Injili vizuri tu kama mhubiri mwingine anavyoweza kufanya. Hilo ndilo hasa, Yesu alisema hivyo. Biblia inafundisha hilo. Naam, bwana. “Nijaposema kwa lugha za wanadamu na malaika, nijapotoa mwili wangu uchomwe moto kama dhabihu, nitoe mali yangu yote kuwalisha maskini, ni—niwe na imani kuhamisha milima, nifanye mambo yote haya, nihubiri katika Jina Lake, nitoe pepo katika Jina Lake,” alisema, “si kitu mimi.” Kwa hivyo, angeweza kutenda hayo, na “si kitu.” Mnalipata hilo wazo?

¹⁴⁰ Sasa, jambo la kufanya ni, kutoka ndani ya moyo wako, kuwa Mkristo, sasa ingia kwenye mlango mwembamba. Kwa maana, njia ni pana ambayo huongoza kwenye maangamizi, nao mamilioni mara mamilioni katika kizazi hiki cha waaminio wataingia mle. Kwa sababu, mlango ni mwembamba, na njia imesonga, ni wewe tu na Kristo peke yenu.

¹⁴¹ “Njia imesonga iendayo Uzimani, na ni wachache tu watakaoiona.” Sasa, hayo ni Maneno ya Bwana wetu. Jamani! Yeye alikuwa anafanya nini? Akiwa amesimama pale, akitambua mawazo yao.

¹⁴² Naye akasema, “Yeye ni Beelzebuli. Vema, anawezaje Yeye kuwa Mungu? Yeye ni Mwanadamu! Hii hekima ilitoka wapi?” wakasema katika mji Wake Mwenyewe.

¹⁴³ Wakati unapoingia jijini hapa, inaonekana kama... Sisemi hili kwa kuwadharau ninyi watu; nyinyi ni Wakristo, mnanipenda. Unaingia jijini hapa, na yaonekana kana kwamba nguvu za Shetani zinakuangusha chini. Mahali hapa pamehukumiwa. Jiji hili limehukumiwa.

¹⁴⁴ Billy Graham alisema nini alipoingia Louisville? Alisema hapo ndipo “mahali palipo na nguvu za pepo sana kuliko mahali pengine” alipowahi kuona maishani mwake. Akaliweka gazetini, akasema, “Waweza tu kuhisi kule kudhulumiwa na ibilisi.”

¹⁴⁵ Hakika, ningekuhisi. Kwa nini? Hapa ni nyumbani kwangu. Wakati Yesu aliporejea nyumbani Kwake Mwenyewe, Yeye alisema miujiza mingi hangeweza kufanya, kwa sababu ya kutokuamini kwao. Akasema, “Nabii hakosi kupata heshima, mhubiri, isipokuwa iwe ni katika ninii yake—katika nchi yake mwenyewe, miongoni mwa watu wake mwenyewe.” Mnaona? Huwezi kujizuia, Maandiko yanasema hivyo. Mnaona?

¹⁴⁶ Sasa, wakati unapotembea mjini hapa! Na usiniambie mimi singejua. Nakutana na watu ambao hunipa mkono na kusema, “Loo, Ndugu Branham, nakupenda.” Na unajua huo ni uwongo! Unajua ni uwongo. Iwapo Mungu anaweza kuniambia upambanuzi wa moyo, kwa nini asiweze kuniambia hilo?

¹⁴⁷ Hakika, na kati ya watu wako mwenyewe jijini! Wakati wanapokuona, kasema, “Vema, wajua, nimeona ambapo ninii fulani-fulani. . .”

“Wapi? Ilikuwa wapi?”

“Juu pale. . .”

“Huh! Tunamjua jamaa huyo!”

¹⁴⁸ Unahisi jambo hilo. Hebu nikwambie, hebu acha mtu fulani aje nyumbani kwako ambaye hakupendi sana, akae nyumbani mwako kidogo tu na upate hisia hiyo ya ajabu. Zidisha hali hiyo mara kumi na nne elfu sasa, ndipo upate kile ninachozungumzia. Halafu unafika mahali ambapo kila mtu anakupenda, hisi hiyo ya kukaribishwa, ninii tu, loo, jamani, nawe ungeweza kukaa tu hapo daima, unaona. Ndivyo ilivyo, unaona, ni roho. Na watu hawajui ni kitu gani, wanashangaa ni kwa nini watu wamepotoka sana.

¹⁴⁹ Nini kinawafanya wanawake wazuri, nini kinawafanya wanawake wazuri wavae nguo za aibu na kutoka huko nje? Nini kinawafanya, hata sasa wakati bado kuna baridi, wasichana wadogo wa miaka kumi na sita, huku wamevaa nguo ambazo haimpasi kuvaa mbele ya mama yake, na nje huko barabarani? Ni kwa sababu, si mtoto huyo (mtoto huyo hajui lililo bora), lakini ni kwa sababu mhubiri fulani katika mimbara ameshindwa kushikilia wajibu wake. Hiyo ni kweli kabisa. Hakika. Wanawake wanakwenda barabarani, na wote

wamevaa kizinifu na mambo kama hayo, na wenye dhambi wanawaangalia na huyo mwanamke hajui kwamba kwa kweli ana hatia sawasawa tu kama kwamba amezini na mwanamume huyo. Yesu alisema hivyo! Yesu alisema, “Kila mtu amtazamaye mwanamke kwa kumtamani, amekwisha kuzini naye moyoni mwake, na itambidi kujibu kwa ajili ya jambo hilo siku ya hukumu.” Mlango ni mwembamba, na njia imesonga!

¹⁵⁰ Najua mnafikiria mimi ni mtu mgumu. Mimi si mgumu! Mimi ni ndugu yenu, nami ninawapenda.

¹⁵¹ Ikimbie ghadhabu ijayo! Nenda msalabani na ulie mpaka moyo wako umejazwa na Roho Wake, ambaye atauguza mgongo wako kwa kila kitu cha ulimwengu, na uenende kitauwa mbele Zake, huku moyo wako ukiwaka kwa ajili Yake. Upendo! Si wajibu. Kristo si wajibu, kumtumikia Kristo, upendo ndio unaomtumikia Kristo. Unakushurutisha, unakushurutisha, mpaka kila pigo la uhai wako hupiga pamoja Naye. Hapo ndipo uonapo dhambi.

¹⁵² Na Yeye alilia juu ya dunia. Ilimhuzunisha Mungu katika siku za Nuhu, wakati alipoona ile mioyo. Na Yesu aliketi juu ya kilima, akasema, “Yerusalem, Yerusalem, ni mara ngapi nimetaka kuwakusanya pamoja, lakini saa yako imefika na nyumba yako imeachwa hali ya ukiwa.”

¹⁵³ Ndivyo itakavyokuwa katika Kuja kwake Mwana wa Mungu, mioyo ya mwaminio halisi wa kweli imevunjika. Yeye anaona sasa hivi kwapaswa kuwe na uamsho ukiisambaa nchi hii. Inawezekanaje kupitia kundi la wana wa haramu? Inawezekanaje, wakati ambapo kwanza wamelaaniwa?

¹⁵⁴ Ufalme wa Mungu ni kama mtu aliyetupa wavu baharini, na, alipouvuta, alipata kasa, makobe, nyoka, vyura, samaki wachache. Haikuwa kazi yake kuamua ni gani, aliyetupa tu ufukoni. Hivyo ndivyo Injili hufanya. Hivyo ndivyo Billy Graham, Oral Roberts, mimi mwenyewe, na wahubiri wengine wote ambao wanahubiri Injili, wanautupa, wanauvuta, “Hao hapo, Bwana.” Lakini tunafanya nini kila wakati? Tunaona, kabla ya kurudi tena, wamerudi moja kwa moja kwenye kidimbwi tena. Ni kitu gani? Tangu mwanzo, alikuwa kasa. Hilo halikumbadilisha, kushikwa katika wavu wa Injili. Alikuwa kasa tangu mwanzo. Alikuwa kobe tangu mwanzo. Alikuwa nyoka tangu mwanzo. Alikuwa mnafiki kabla ya kuja kanisani. Hata hakuwa na shauku ya kuacha ulevi wake na kucheza kamari, na kuvuta sigara na kudanganya, na kuiba. Aliingia tu kwa sababu aliogopa jehanamu. Unajifanya wa huko zaidi, wakati unapofanya hivyo. Hiyo ni kweli. “Mlango ni mwembamba, na njia imesonga, nao watakaonia ni wachache.”

Hebu tuombe.

¹⁵⁵ Bwana, ee, nichunguze, Bwana. Hukumu kesi yangu sasa hivi, Bwana. Usiniache inibidi kuja mbele ya hukumu mbele

Zako, baada ya kuhubiri namna hii. Loo, kama kuna kitu chochote kichafu ndani yangu, Bwana, kiondoe, tafadhali! Tunaona siku ambayo tunaishi, wakati ambapo wanaume na wanawake wanakuwa wagumu mno. Wanaona aibu. Ulisema wakati mmoja, “Hakuna hata haya miongoni mwa binti wa Sayuni.” Adabu zao zimeondolewa kwao mpaka hata hawaoni aibu tena. Ee Bwana, wazia hilo! Na ujue kwamba ile saa huko ng’ambo inamalizia kuhesabu, dakika moja tu au mbili zaidi, na maangamizi makuu yatakuja, basi aliye mchafu na azidi kuwa mchafu.

¹⁵⁶ Mungu, tuamshe sisi sote asubuhi hii. Tutikise, Bwana! Twaona ishara zikitokea. Tumefungua macho yetu kujua hilo. Tunaona mamilioni, mamilioni, Bwana, ambao wamegeuka na kwenda zao. Nashangaa, nifanye nini, nifanye nini, Ee Bwana? Kuna kitu chochote, Bwana? Kama inahitaji kuhubiri zaidi, maombi zaidi, jambo lolote zaidi, nisaidie, Bwana, ili nipate kuwaletea watu Ujumbe. Nifanye nini? Lakini wanaendelea kuukataa. Wewe unatenda ishara Zako kubwa na kutenda maajabu Yako, na hata hivyo watu wanaendelea mbele tu. Ni kwamba Maandiko Yako hayana budi kutimia, je, ni wakati ambapo “Hakuna mtu awezaye kuja Kwangu asipovutwa na Baba Yangu, na wote ambao Baba amenipa Mimi watakuja Kwangu”? Bwana Mungu, tujalie asubuhi hii kwamba watu wataamka na kuona ishara hii ya mwisho wa dunia. Naomba, Mungu, kwamba Wewe utawajalia watu jambo fulani.

¹⁵⁷ Bariki maskini watu hawa waliopo hapa asubuhi ya leo. Mungu, anzia na Ndugu Neville, Bwana. Uponye mwili wake. Ni mgonjwa asubuhi ya leo, Bwana, tumbo limechafuka. Naomba kwamba mkono Wako wa uponyaji utakuwa juu yake. Chochea nafsi yake.

¹⁵⁸ Mungu, enenda miongoni mwa kusanyiko hili. Kuna wanaume na wanawake wanaoketi hapa ambao huenda nisiwaone tena hadi siku ile ya hukumu, ndipo itanibidi kutoa hesabu. Lakini nimesoma Neno Lako, “Mlango ni mwembamba, na njia imesonga, nao watakaonia ni wachache.” Ee Bwana, jalia hawa wawe wale “wachache,” baadhi yao, je, utafanya hivyo, Bwana? Jalia kwamba kila mtu hapa.

¹⁵⁹ Ninaomba kama mwanadamu awezavyo tu kuomba. Bwana, watu hawa wangefanya chochote kwa ajili yangu, kadiri ya kunisaidia mimi. Kama ningekuwa na njaa, wangenilisha. Kama ningehitaji suti, wangeinunua. Wangekwenda pamoja na kuninunulia motokaa, kuhubiria Injili. Wangetenda chochote kwa njia hiyo. Ee Baba, chunguza nafsi zao asubuhi ya leo, tafadhali zichunguze, na hebu wao wazichunguze mbele Zako. Mimi sijui, ninatumaini ya kwamba kila mmoja wao yuko katika wale Wateule. Nami niweke humo, pia, Bwana. Na kama kuna sababu yoyote ndani yangu ya kwamba nisingekuwapo hapo, Bwana, Wewe nifunulie tu, nitaisahihisha sasa hivi. Nataka

kuwa na hakika, Bwana, kwamba asubuhi ile hakutakuwa na matatizo pale mtoni. Nataka kuingia siku ile. Nami sijui hiyo itakuwa lini, yaweza hata iwe leo. Kwa hiyo, nisaidie kujua, wasaidie watu hawa kujua.

¹⁶⁰ Na wakati tuonapo mioyo yetu haijali! Loo, tunafurahia Ujumbe mzuri kusikiliza kwenye redio, au kwenda kanisani. Tunathamini Ujumbe mzuri. Hatujali kuzungumzia habari za Yesu mahali fulani. Lakini, Bwana, hivi dhambi ni mzingo mno kwetu, nayo huleta machozi machoni mwetu, tukiugua na kulia na kusimama kuipinga, kadhalika, machukizo yanayofanyika jijini? Bwana, jalia Malaika wa Mungu aone hilo juu yetu, na kututia alama. Tujalie, Bwana.

¹⁶¹ Na uje, Bwana Yesu, sasa na uitayarishe mioyo yetu, na utupe ishara Zako za kweli kwamba uko katikati yetu, ili tuweze kujua kwamba tunapokea—tunapokea ishara ya mwisho kabla ya mwisho wa kizazi hiki.

¹⁶² Na tunaona uharamu, wakati wanaume wanaoishi nchini wana watoto waliozaliwa na wake wa waume wengine, na—na wasichana wadogo mitaani, na mamia wanafukuzwa kutoka shuleni kila mwaka na matineja wanakuwa waja wazito, na hakuna heshima, na jinsi ambavyo wanawake wanakuwa sumu, wenyewe, kwa kuvuta sigara na—na kunywa pombe, na televisheni na kadhalika ambayo yanapotosha akili za watoto. Ee Bwana, itaendelea kwa muda gani? Na Wewe, Mungu Mtakatifu!

¹⁶³ Ee Baba, na—najisikia hali isiyo ya kawaida leo kwamba jambo fulani lazima lifanywe haraka, Bwana. Sijui la kusema, bali naomba, Bwana, kwamba Wewe utaweka katika mioyo yetu la kutenda. Tujalie mambo haya, Bwana. Tunaomba hayo katika Jina la Yesu. Amina.

¹⁶⁴ Saa imekaribia. Kila mtu mwenye busara ambaye ana akili, anajua kwamba kitu fulani kinakaribia kutukia. Hakuna mtu katika jengo hili, mwenye akili timamu, ila anayejua kwamba ulimwengu huu hauwezi kusimama chini ya hali hizi.

Hatuwezi kuyastahimili, enyi marafiki. Hakuna hata kitu kimoja, kama mchungaji wenu na ndugu yenu, hakuna hata jambo moja ambalo naweza kukuelekezea asubuhi hii ila kwa Yesu Kristo. Hakuna kitu nijuacho. Hebu fikiria tu mambo ambayo yametabiriwa kuja kabla ya Unyakuo kutukia, kila kitu nikijuacho tayari kimetimia.

¹⁶⁵ Unasema, “Na alama ya mnyama je?” Hiyo itakuja katika ile Dhiki. Kanisa litakuwa limekwisha kuondoka wakati huo. Haitabidi kuwatia hawa alama, hawa watakuwa wamekwisha kwenda, mnaona. Kutiwa alama kunaendelea sasa. Kutiwa alama ni kule kuonyesha, ile chapa. Mkimbilieni Mungu, mkimbilieni upesi!

¹⁶⁶ Nashangaa asubuhi ya leo, wakati tukiwa tunangojea hapa kidogo. Nami najihisi kama mnavyohisi. Ni—ninaweza kuhisi kujisikia kwenu, kila mmoja wenu akijaribu kufikiria, “Ee Mungu, nichunguze!” Hivyo ndivyo ninavyojisikia, pia. Ninatambua kwamba Jumbe hizi za namna hiyo, rafiki, si maarufu miongoni mwa watu. Unawahukumu na unahu... una—unawashusha tu. Mtu fulani hana budi kufanya jambo hilo. Laiti ingekuwa labda mtu mwingine. Lakini kama ikiniangukia kulitenda, kama ikinibidi kuwa ndiye mama msuguaji, acha nisugue. Kama mimi... Daudi alisema, “Afadhali niwe mkeka wa mlango kwenye Nyumba ya Mungu, kuliko kukaa katika hema pamoja na dhambi.” Hilo ni kweli. Lolote lile Mungu akutakalo ufanye, lifanye. Usione aibu. Kama kuna...

¹⁶⁷ Pia, kumbuka, najua hilo ni jambo kubwa. Wasema, “Ndugu Branham, unasema nafsi nane tu zingeokolewa?”

¹⁶⁸ Sijui ni wangapi wataokolewa, siwezi kukuambia. Lakini nasema kitu kimoja: watakuwa wachache sana, katika siku kama hii. Hebu fikiria tu, katika siku ile ambayo Yeye alikuwepo, ni wangapi waliokolewa. Wazia siku za Nuhu, na siku za Lutu—Lutu, na hao wote, Yeye alisema, “Ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwake Mwana wa Adamu, sababu, mlango ni mwembamba, na njia imesonga.” Unaona, unaingia wewe binafsi, pamoja Naye, na ni hivyo tu. Unaona? “Na bali ni wachache watakaoiona.” Wangapi wanaamini hiyo ni Kweli ya Injili? Yesu Kristo alisema hivyo, “Wachache ndio watakaoiona.” Wachache sana. Uwe mmoja wa hao wachache. Najua hilo ni gumu, linahangaisha. Na linanipa shida kulisema, nikiwa na upendo wa kibinadamu kwa ajili yenu, lakini upendo wa Mungu unanishurutisha kuwaambieni.

¹⁶⁹ Sasa, Roho Mtakatifu yeye yule aliyetenda katika siku za Ibrahimu, aliyetenda katika siku za Kristo, aliahidi kuwa hapa kutenda kitu kile kile. Yupo hapa. Sasa, kama nimewaambia Ukweli, Mungu anawajibikia Ukweli huo.

¹⁷⁰ Nisipotimiza neno langu, mimi si mtu mwaminifu kwa neno langu. Kama hutimiza neno lato, wewe si mwaminifu kwa neno lato. Sasa, naweza kukuahidi kitu na nisiweze kukifanya, lakini—lakini nitakuja nikuambie. Kama unaniwia kitu fulani, na ninajificha usinione, mimi ni mnafiki. Kama nikija nikwambie, “Unaniwia, lakini siwezi kukulipa, lakini nitafanya niwezavyo,” basi unanisamehe na kunisaidia. Unaona?

¹⁷¹ Sisi sote tunawiwa kitu fulani na Mungu. Tunawiwa na Yeye maisha yetu. Hebu na tuwe waaminifu kuhusu hilo. Jitokeze na kusema... Usiseme, “Vema, sasa angalia, mimi—mimi ni Mpresbiteri. Mimi ni Mmethodisti. Mimi ni Mpentekoste. Mimi ni Church of God. Mimi ni Mnazarayo. Mimi ni Mpilgrim Holiness.” Usiwazie hayo! Kutakuwa na mamilioni ya hao kuzimuni. Wewe kuwa Mkristo, katika Kristo.

¹⁷² Wangapi watasema, “Ndugu Branham, nikumbuke katika maombi sasa, nataka kuinuka”? Mungu akubariki.

¹⁷³ Bwana, Wewe unaona mikono yao. Saa imewadia, Roho Mtakatifu aliye mkuu ametuliza jengo hili asubuhi hii. Ninahisi Uwepo Wako. Natambua kwamba Wewe upo hapa kuliheshimu Neno Lako, “Mimi Bwana nimepanda, na nitalitilia maji mchana na usiku, asije mtu akalinyakua kutoka mkononi Mwangu.” Wewe ulituma Neno Lako kutimiza kusudi fulani, nalo lita—litafanya hivyo, Bwana. Maandiko yanasema kwamba Wewe ni yeye yule jana, leo, na hata milele.

¹⁷⁴ Hawangeamini, hao watu katika siku Zako hawangeamini kwamba Roho Mtakatifu alikuwa ndani Yako. Na ulijifanya Mwenyewe (ukiwa Mwanadamu) Mungu, ambapo, Wewe ulikuwa yule Mwana wa Mungu aliyezaliwa na bikira ambaye alikuja duniani kutukomboza sisi kutoka kwa dhambi zetu. Na kwa sababu kwamba waliona Roho wa Mungu ndani Yako, walijaribu kumfanya kitu kingine. Na Wewe uliwaambia, Bwana, “Si Mimi ambaye hutenda hizi kazi, ni Baba Yangu ambaye anaishi ndani Yangu. Yeye hutenda hizi kazi. Kama mlimwita Ibrahimu ‘baba’ yenu. Ibrahimu aliiona siku Yangu.” Hakika, aliiona, alipokuwa amesimama karibu Naye, alimwona Huyo akifanya kazi zile na ishara. “Aliiona siku Yangu na akaifurahia.” Kasema, “Mwapotea, kwa kuwa hamyajui Maandiko wala Nguvu za Mungu, jinsi ambavyo Mungu aliweza kumtia uvuli bikira, na kuzaa Mwana (kwa uzao wa bikira) na kuishi Mwenyewe katika ukamilifu wa Nguvu Zake, ndani ya Mtu huyo mmoja.”

¹⁷⁵ Na jinsi Yeye alivyoweza kuchukua Damu ile ile kutoka katika Mwili ule ambao Yeye aliutoa kama Dhabihu, na kutakasa watu ambao Mwenyewe angeweza kuishi ndani yao, kuendeleza kazi Yake hata ukamilifu wa dahari! Ee Mungu, waamshe watu wapate kuona hilo. Tujalie. Okoa kila mmoja ambao wameinua mkono wao. Takasa mioyo yao. Bwana, mikono yangu imeinuliwa. Nitakase, Ee Bwana. Hii ni nyumba ya masahihisho. Hapa ni mahali ambapo tunapaswa kuoshwa. Jalia Roho Mtakatifu atusafishe asubuhi ya leo, na atutakase na uozo.

¹⁷⁶ Tunaomba, Bwana, kwamba hapatakuwepo mtu atakayeondoka hapa ila atakayejazwa na Roho Wako. Labda hapatakuwa na mhemko hata mmoja kutoka nje wakati inapotukia. Lakini, Bwana, ingia ndani, uvute na kuondoa ganda na utuonyeshe kile tulicho, Bwana. Tujalie. Na kisha utujaze na Roho Wako, kwa moyo ambao ni wa kweli na safi. Na wakati huu wa mateso na majaribu mazito, Wewe utazidi kuwa mzuri na wa kupendeza zaidi kwetu tunapoendelea na safari, tuingojea siku ile. Wakati machozi yakitiririka mashavuni mwetu, kwa ajili ya dhambi za jiji hili, jalia Roho Mtakatifu atazame chini na aseme, “Yupo mmoja ambaye naweza kumtia

alama, ni mwanangu Mimi, ni binti Yangu.” Tujalie, Bwana. Hebu lionekane miongoni mwetu leo. Tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

Nifikapo mtoni mwishoni mwa siku,
Na pepo za mwisho za huzuni zimekwisha
vuma;
Patakuwa na Mtu akingojea ambaye
atanionyesha njia,
Haitanilazimu kuvuka Yordani peke yangu.
Haitanilazimu kuvuka Yordani peke yangu,
Yesu alikufa apate kupatanisha dhambi zangu
zote;
Nitakapoona lile giza, Yeye atakuwa
akingojea,
Haitanilazimu kuvuka Yordani peke yangu.

¹⁷⁷ Nataka kumjua Yeye sasa. Nishike mkono, Bwana wa thamani, niongoze, nijalie kusimama. Nijalie kusimama hapa, Bwana, dhidi ya kila kitu kinachoitwa kosa, kila kitu kinachoonekana kuwa kibaya. Sijali mtu yeyote anasema nini, jalia nisimame, Bwana. Wakati nimefanya yote niwezayo kufanya, nisaidie kusimama. Nishike mkono univute nivuke jambo hilo, Bwana. Tenda jambo, jalia nisimame. Wakati mambo hayo yajapo, na hazina za ulimwengu huu na fahari yake yote na utukufu wake; nipofushe macho yangu nisiyaone hayo, jalia nimwone tu Yeye, Yule aliyenifia. Hata ikinigharimu kila rafiki niliye naye, hata ikinigharimu kila kitu nilicho nacho; hilo halimaanishi kitu, natoa vyote juu ya madhabahu. Jambo ndilo hilo, nijalie nidumu mwaminifu. Na siku moja wakati pumzi linavuma dhidi ya uso wangu, nami najua kwamba moyo wangu umeenda na siku zangu zimekwisha, na wakati wangu umefika na kadi yangu imeondolewa kwenye rafu, nataka nisivuke Yordani peke yangu. Yeye atakuwepo pale. Naam. Nitakapoona lile giza, Yeye atakuwa ananingojea, haitanilazimu kuvuka Yordani peke yangu. Kama nitamtetea sasa, Yeye atanitetea wakati huo. Nitaishi kwa ajili Yake Yeye aliyenifia, jinsi maisha yangu yatakavyokuwa ya furaha. Hivyo ndivyo ninavyotaka kusimama.

¹⁷⁸ Nadhani kuna wagonjwa hapa. Hivi alisambaza kadi zozote? Nilisahau. Walisambaza kadi? Kadi zozote zimetolewa? Kuna mtu yeyote aliye na kadi za maombi? Hapana.

¹⁷⁹ Ninamngojea tu Roho Mtakatifu. Kama mkiamini tu, muwe tu na imani, msitie shaka. Kama Mungu atanifunulia matatizo yenu. . . Yoyote yale, sijui; kama ukiinua mkono wako, hunijui mimi nami sikujui wewe. Basi kama Mungu atafunua hapa, utaamini ni Malaika yeye yule ambaye alileta Ujumbe kabla tu ya maangamizi huko nyuma, itakuwa ni Malaika yule yule ambaye alikuwa anauleta sasa hivi kabla ya maangamizi

mengine. Utaamini jambo hilo? Kama utaamini, inua mkono wako. Vema. Vema, Bwana na alijalie hilo.

¹⁸⁰ Ameketi karibu nami. Kuna mwingine aliyeketi karibu nami, ni Bibi Snyder hapa, au huyu Bibi Murphy hapa, ndilo jina lake, akiwa ameketi papa hapa. Ninawajua.

¹⁸¹ Simjui mwanamume huyu, yeye ni mgeni kwangu mimi. Lakini Mungu anamjua. Kama Mungu atalifunua sasa, ni wangapi wenu wanajua kwamba si. . .

¹⁸² Msinitazame mimi. Jamani, mimi ni mshamba wa Kentucky, kuhusu jambo hilo. Si—sina hata elimu ya kutosha, ni vigumu, ku—kuandika jina langu mwenyewe. Lakini kuna jambo moja nijualo, ninamjua Yeye. Na hilo, hilo—hilo tu ndilo ninalojali kujua. Sasa, usi—usijali sarufi yangu.

¹⁸³ Na huenda ukafikiria kwamba mahubiri yangu asubuhi hii hayakufaa na kadhalika, hebu yalinganishe na Biblia wakati mmoja na uone kama hulengi sawasawa kwenye shabaha. Angalia kama darubini yako hailengi ndani wakati—wakati unapoelekeza mle. Usiyalinganishe na mawazo yako mwenyewe, lakini yalinganishe na lile ambalo Yeye alisema. “Mlango ni mwembamba, njia imesonga, nao watakaonia ni wachache; maana njia ni pana iendayo upotevuni, na mlango ni mpana, na wengi wataingia humo,” mamilioni mara mamilioni wataingia humo. Mmoja katika milioni moja ndivyo labda itakavyokuwa. Haya basi. Hivyo ndivyo Yeye alivyosema. Sasa, Yeye kamwe hakutoa idadi hiyo, lakini alisema, “Kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu, watu wanane. Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, watatu.” Kutoka katika kundi zima, watatu waliokoka, kwa moto. Ndivyo itakavyokuwa!

¹⁸⁴ Sasa, kama mtu yeyote ni wa kiroho kweli, nataka mumwangelie mwanamume huyu aliyeketi hapa, ananiangalia kwa makini sana. Aliinua mkono wake, simjui; sijawahi kumwona, wala sijui chochote kumhusu. Ameketi tu hapo akiniangalia. Lakini, unaona, anafanya mawasiliano, anaomba. Sasa, hiyo ni kweli. Sasa, kama Bwana ataniambia. . . Mtu huyo aliyeketi mbali hivyo kutoka kwangu, na hii ni mara yetu ya kwanza kukutana, naye huyo hapo ameketi. Kama Bwana atanifunulia kile ambacho yeye—kile yeye. . . Si—siwezi kumponya. Siponyi, siwezi kufanya hilo, sababu Mungu tayari ametenda hilo. Lakini ingeongeza imani yenu. Kila mtu anaona sasa, Yeye yupo papa hapa, Roho yule yule tu. Pia kumbukeni, Yesu aliahidi hili, kabla ya wakati wa mwisho. Sikuzote imekuwa ndiyo ishara ya mwisho.

¹⁸⁵ Hivi majuzi, mimi na Leo tulikuwa tumeketi barabarani, na baadhi yetu tukizungumza. Na ninaendelea kuhisi kuna badiliko linakuja, badiliko linakuja. Wakati tulipozungumza habari zake, halitakuwa badiliko katika huduma yangu, sababu haiwezi kuwa zaidi, lakini litakuwa badiliko ndani yangu.

Sikuzote nimekuwa mnyonge na kuwaachia watu tu waniongoze na kunielekeza, na kunituma *huku* na *kule*. Kama ningetenda jambo aliloniambia Bwana kutenda muda mrefu uliopita, nisingekuwa katika matatizo niliyo nayo leo. Nitaenda zangu juma hili lijalo kuwa peke yangu na Mungu. Naam, bwana. Si—sina budi kusikia kutoka Mbinguni. Sitaki kuwa mnyonge, nataka kusimama juu ya imani yangu mwenyewe.

¹⁸⁶ Mwanamume huyo, inaendelea kurudi kwake moja kwa moja, ameketi huko nyuma, maana mtu huyo anaamini, yeye hakika anaamini. Naangalia wasikilizaji kila mahali, na inarudi moja kwa moja kwa mtu huyo. Ana haja, ana mzigo, lakini ana mzigo kwa ajili ya mtu mwingine. Hiyo ni kweli. Unaomba kwa ajili ya mtu mwingine. Unaye mtu mwingine moyoni mwako. Hiyo ni kweli, sivyo? Ni rafiki. Kama nikikuambia rafiki huyo ana tatizo gani, je, utaniamini mimi kuwa ni mtumishi wa Mungu? Ni ulevi. Hiyo ni kweli. Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako.

¹⁸⁷ Unaamini? Mtu fulani hapa aliinua mkono wake, mwanamke nyuma hapa, mtu fulani. Ndiyo. Naam. Hunijui? Mimi ni mgeni kwenu nyote? Siwajui, lakini Mungu anawajua. Unaamini hilo? Kama Mungu atanifunulia kilichoko moyoni mwako, je, utaniamini mimi kuwa ni mtumishi Wake? Bi mdogo, linalokusumbua ni huyo mtoto mchanga hapo. Hiyo ni kweli. Na mtoto huyo mchanga ana upele mbaya sana usoni mwake. Daktari hawezi kufanya chochote kuhusu jambo hilo. Wewe ni mgeni hapa, wewe na mpendwa wako aliyeketi hapo. Unaamini Mungu anaweza kuniambia wewe ni nani au unatoka wapi? Unaamini jambo hilo? Ungekubali uponyaji wa mtoto huyo mchanga kama Yeye angemponya? [Mwanamke huyo anasema, “Ndiyo.”—Mh.] Vema, waweza kurudi Somerset, Kentucky, mahali unakotoka. Na uamini kwamba atapona, upele wako utamwacha huyo mtoto kama unaweza kuamini hilo.

¹⁸⁸ Nilipotaja neno hilo, mtu fulani anayesimama pale nyuma ukumbini, kutoka Somerset, Kentucky, akiomba, ana ugonjwa wa moyo. Unaamini kwamba Mungu atakupua afya? Kama ukiamini kwa moyo wako wote, na uamini kwamba Mungu atakuponya na kukupa afya.

¹⁸⁹ Hapa, hapa pana, naamini mkono wa mtu fulani uliinuliwa mahali fulani hapa, papa hapa, mwanamke. Ndiyo, niliona mkono wako. Mimi ni mgeni kwako, mama? Sikujui. Hatujawahi kukutana. Unaniamini mimi kuwa ni mtumishi Wake? [Mama huyo anasema, “Ndiyo.”—Mh.] Unaamini? Una mzigo moyoni mwako, au jambo fulani. Unaamini kama Mungu anaweza kunifunulia hilo mimi, unaamini ni Roho yule yule ambaye alikuwa ndani ya Kristo? Mumeo anaketi hapo, anaamini kitu kile kile, pia? Utaamini jambo lile lile? Ni kuhusu msichana wako mdogo aliyeketi karibu nawe hapo. Hiyo ni kweli, ana kansa.

Lakini unaamini kwamba Mungu atamponya? Kama unaamini, inua mkono wako. Vema, weka mikono yako juu ya mtoto huyo.

¹⁹⁰ Bwana Yesu, katika Uwepo wa Roho Wako, ninalaani pepo huyo ambaye anamwua mtoto huyo. Naweka, kwa imani, Damu ya Yesu Kristo kati ya mwuaji huyo na mtoto huyu. Jalia aishi. Amina.

¹⁹¹ Mwamini Mungu. Usitie shaka. “Kama unaweza kuamini, yote yanawezekana.” Kama unaweza kuamini, mambo yote yanawezekana. Barabara.

¹⁹² Mtu mwingine nyuma kule aliinua mkono wake, mahali fulani, wewe, mama mmoja kule mwisho. Unaniamini mimi kuwa ni mtumishi wa Mungu? Sikujui, wewe hunijui. Unaamini kwamba Mungu anaweza kunifunulia tatizo lako ni nini? Utamkubali Yesu kuwa Mponya wako au Mpaji, lolote lile—lolote lile. . . ? Unaamini basi? Vema, basi huo ugonjwa wa neva ambao umekuwa nao, huo ndio uliokuwa nao. Kama jambo hilo ni kweli, simama kwa miguu yako, kama hilo ni kweli, ili watu waone tu kwamba ni kweli. Vema, ugonjwa utakuacha sasa. Nenda nyumbani ukawe mzima. Mungu akubariki.

Wewe unatoka Kentucky, pia. Uh-huh, hiyo ni kweli.

¹⁹³ Mama huyo aliyeketi karibu nawe anatoka Kentucky, pia. Yeye, pia. Sikujui, sivyo? Lakini naweza kukuambia kuwa una shida fulani. Kama ninaweza kukuambia tatizo lako, utamkubali Kristo kama Mponyaji wako? Iko kwenye nyonga yako. Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako, juu kabisa ili watu waweze kuona. Vema, nenda nyumbani sasa, utakuacha. Imani yako inakuponya.

Nakusahi kuamini. Naisahi imani yako kuamini.

¹⁹⁴ Huyu hapa ameketi mama mmoja, anaomba, ameinua lesu yake usoni mwake. Sikujui. Mungu anakujua. Unatoka Joliet, Illinois, na una uvimbe. Hiyo ni kweli kabisa. Waweza kushangaa. . . (Ndiyo, huyo ni yule—huyo ni yule mwanamke aliyeletwa na Rosella. Hiyo ni kweli. Ngoja, aliniambia jambo hilo, lakini hakujua kamwe kwamba sikumjua mwanamke huyo. Hiyo ni kweli. Inatokea tu kuwa imani ya yule mwanamke ilikuwa kubwa.) Nitakwambia kitu kimoja u—unachojua kwamba sijui. Unamwombea mtoto huyu aliyeketi hapa mwishoni mwa kiti, ambaye ni mgonjwa. Huyu ni mtoto wako. Hiyo ni kweli. Amina. Unajua sikujua hilo.

¹⁹⁵ Huyu hapo, ni Roho Mtakatifu! Unamwamini? Unamkubali Huyu? Basi kama hilo ni kweli, nililosema kuhusu “mlango ni mwembamba, na njia imesonga” ni kweli. Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, yupo papa hapa sasa. Roho wa Mungu aliye hai yupo papa hapa. Mnamwamini Huyu? Basi, kuwaonyesha kwamba mimi si mtu anayeponya, mimi si mponyaji, lakini Roho wa Mungu alinichagua tu kujidhihirisha Mwenyewe. Sina elimu. Sina maarifa ya chochote. Lakini ni Roho Wake ambaye

anatenda jambo hilo, mnaona, na Yeye anataka ninyi mjue kwamba nimewaambia Kweli.

¹⁹⁶ Hii ni Kweli, kwamba Yesu Kristo anamfanya kila mmoja wenu mzima sasa hivi kama mtaamini hilo. Sasa kama tu... Kama lilifaulu huko Kingston, ambalo wale wamishenari, au yeyote huko nyuma, aliona Hiyo ikifanya kazi huko Kingston, kwa maelfu wakiponywa, kwa nini isifanikiwe hapa katika Marekani hii ambako tuna jambo hilo namna lilivyo sasa? Kwa nini tusiliamini? Kwa sababu hatuwezi kuvuka hayo mawimbi madogo huko ng'ambo. Mnaamini hilo? Inueni mikono yenu.

¹⁹⁷ Sasa, mikono hiyo hiyo, iweke juu ya mtu fulani karibu nawe, hebu nimwombee kutoka papa hapa, na usiwe tena na shaka moyoni mwako, hili litaumaliza.

¹⁹⁸ Loo, jamani, Ndugu Neville! Jinsi nimetamani, jinsi nimeomba, jinsi mimi... Huenda mkafikiri nimerukwa na akili; sijarukwa na akili. Najua kwa hakika mahali nilipo. Laiti ningeliweza tu kuwapa kitu hiki kidogo! Mnatambua kwamba Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, hapa katikati ya watu asubuhi hii, sasa hivi, yupo sasa hivi, akijionyesha Mwenyewe?

Vema, unasema, "Ndugu Branham, *wewe* ulisema jambo hilo."

¹⁹⁹ Nilisemaje? Sikujui wewe. Kuna mwanamke mwingine aliye na TB. Umeponywa, dada. Akubariki. Samahani, ulikuwa unamwomba mwanamke aliye na TB, maana ni mwanamke mwenye mvi. Ndiyo. Vema, amini hilo. Vema. Yupo hapa. Ni Uwepo Wake.

²⁰⁰ Sasa, hili hapa alilosema Yeye, "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio. Wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya." Anawezaje Yeye kusema uongo? Unaona, siyo juu Yake, siyo juu yangu, sasa ni juu yako. Sasa wewe amini.

²⁰¹ Ninamwangalia maskini mwanamke aliyeketi nyuma kule sasa hivi, ana imani kubwa sana. Yeye na mumewe wamekuja kwa Bwana hivi karibuni. Aliketi papa hapa katika mkutano huu, alikuwa na henia ambayo daktari alikuwa amfanyie upasuaji hapo kabla, na mtoto wake alikuwa karibu kuzaliwa. Na daktari alikuwa amfanyie upasuaji baadaye, lakini yule mtoto alizaliwa nao hawawezi kuona hiyo ngiri tena. Yote imetoweka. Unaona? Kwa nini? Aliketi tu kama... Hakuja hapa jukwaani namna hiyo. Aliketi tu nyuma kule na akaamini. Hiyo ni kweli, Bibi Green, naamini ni kweli, kule nyuma? Hiyo ni kweli. Unaona mkono wake? Daktari hawezi hata kuona hiyo henia, yote imetoweka. Kwa nini? Aliamini, akajitokeza tu na kusema, "Ni kweli!"

²⁰² Sasa wewe fanya vivyo hivyo, na kila teso ulilo nalo itabidi liondoke. Mungu, Yule awezaye—Yule awezaye kutuma Kitu katika mwili wa binadamu, kwa ile njozi ya kuumwa na nyoka ambaye alikuwa katika mguu wa huyo mtu, akitia sumu,

kumwua, na anaweza kumkomesha na kumwua papo hapo, ni zaidi sana kiasi gani Yeye anaweza kuua magonjwa mwilini mwako. Kwa sababu, mtu yule alikuwa katika taabu naye ilimbidi apate usaidizi. Yakubidi uupate, pia. La sivyo, utakufa.

²⁰³ Sasa wekeaneni mikono nyinyi kwa nyinyi. Usijiombe mwenyewe, mwombe mtu aliye karibu nawe. Huo ndio Ukristo.

²⁰⁴ Jifunzeni hili, jifunzeni hili, kwamba, unapowatendea wengine, unamtendea Kristo. Unapokuwa mwema kwa mtu mwingine, unakuwa mwema kwa Kristo. Kama ukimtendea mtu mwingine mabaya, unamtendea Kristo mabaya. Loo, jamani!

²⁰⁵ Loo, laiti ningeweza tu kufanya hili liingie, laiti ningeweza tu kuwafanya watu wakione, kile ambacho ninatazama na ambacho ninahisi, na ambacho najua kinaendelea, mnaona. Jinsi Kristo anavyousukuma huo Ujumbe asubuhi ya leo, kuingia moja kwa moja katika mioyo ya watu na kuumba kitu fulani humo; si msisimko, si mhemko (huo hufuatana nacho), bali kuumba imani ya kudumu humo ambayo haitasema, mpe adui nafasi kidogo.

²⁰⁶ Sasa, Yeye atasikia maombi yangu, Yeye atasikia yako. Ninyi ombeaneni sasa, ninapowaombea ninyi nyote.

²⁰⁷ Ee Bwana, wakati huu ulio muhimu sana, tunatambua kwamba hili linaenda kumaanisha tofauti kati ya mauti na uzima, kwa wengi. Nami ninatetemeka katika Uwepo Wako, kwani najua, Bwana Mungu, kwamba lazima niombe kwa moyo wangu wote. Ninatambua ya kwamba hata ikiwa yawezekana kusiwe na mtu mgonjwa miongoni mwetu katika dakika tano zijazo, kwamba kila mtu hapa atatambua kuwa Wewe uko hapa. Hawa hapa wamesimama asubuhi ya leo, Bwana. Wajalie hao watu wainue mikono yao ambao walijua kwamba siwajui, wala sijui chochote kuwahusu. Lakini Roho Wako anawajua. Wewe unajua siri ya moyo wao, ni zaidi sana jinsi gani unajua mateso yao na maumivu yao! Basi, Bwana, na iwe leo, na iwe hata sasa kwamba Roho Wako ataigusa miili yao inayougua. Tujalie, Bwana. Wanaombeana wao kwa wao.

²⁰⁸ Nami naomba, Mungu Mpenzi, kwamba Roho Mtakatifu atalifanya kuwa jambo halisi sana kwao, kwamba hawatakosa kuliamini tena. Na kuna ugonjwa mwingine, Bwana, ambao ni mkuu zaidi kuliko ugonjwa huu wa kimwili, ni ugonjwa wa kiroho. Jalia kila moyo ufunguke.

²⁰⁹ Bwana, inawezekanaje kwamba Wewe ulisimama hapo kando ya Ibrahimu, na ukatenda jambo lili hili, ukamwambia Sara ambaye alikuwa “nyuma” Yako, Maandiko yanasema, “huko kwenye hema alicheka,” na Wewe ukamwambia. Ndipo Ibrahimu akatambua kwamba huyo alikuwa Elohimu, Mungu mkuu. Katika dakika chache Wewe ulikuwa umetoweka mbele ya macho yake.

210 Pia, Bwana, wakati Yesu aliposimama na kufanya jambo lile lile, na kusema, “Mlimwita Ibrahimu ‘baba’ yenu, hata hivyo mnasema mnajua Maandiko.” Kasema, “Mwapotea, kwa kuwa hamyajui Maandiko wala Uwezo wa Mungu.” Nao wakamwita “Beelzebuli.”

211 Lakini Wewe uliahidi kwamba katika siku za mwisho kwamba Wewe ungemwaga Roho Wako tena. Nabii alisema, “Wakati wa jioni itakuwa Nuru.” Na sisi hawa hapa.

212 Wakati ulimwengu huu haramu unayumbayumba chini ya dhambi, kama mlevi anavyopepesuka akienda nyumbani usiku, hivi karibuni utalipuka katikati, hata hakutakuwa na vumbi la volkano, ni vigumu kulipata, litakalosalia. Nasi tunaona wakati ukipita.

213 Ee Mungu, ondoa kila shaka toka kwetu. Tusogeze katika duara lile sasa hivi. Njoo, Roho Mtakatifu. Nyosha mabawa Yako makuu, atamia juu ya maskini wasikilizaji hawa sasa hivi, na hebu ukajaze mioyo yao Mwenyewe, na uwajalie kujua kwamba Wewe upo katika Uwepo wa Kiungu, kwamba ni Wewe, “Mimi ndimi Bwana nikuponyaye magonjwa yako yote.” Basi jalia Uwepo Wako utende jambo moyoni mwao ambalo litawafanya waende kutoka hapa, asubuhi hii, wakiadini kwa yote yaliyomo ndani yao. Pia jalia kila aliye mgonjwa na anayeteseka aponywe.

214 Kwa maana, kama mtumishi Wako, nasimama na kulaani kila pepo, naulaani ugonjwa, namlaani Shetani.

215 Umeshindwa, na wewe si kitu ila mdanganyifu. Nasi tunakushtaki kwa hilo, katika Jina la Yesu Kristo. Na kama mtumishi Wake, nikihubiri Neno Lake na kuwaambia watu Kweli, kwamba wajirekebishe na kujinyosha na Neno la Mungu, nakulaani, ewe Shetani, katika Jina la Yesu Kristo. Mwondokee kila mmoja wa watu hawa ambao wametoka mbali na karibu, wapate kuponywa. Ondoka katika kusanyiko hili na katika watu hawa. Nakuapisha kwa Mungu aliye hai. Na Biblia ilisema, “Kuomba kwake mwenye haki kwafaa sana, akiomba kwa bidii.” Na watu wengi wenye haki wameweka mikono yao juu ya wagonjwa, asubuhi hii hapa. Loo, Shetani, ungetaka kuwafanya wafikirie ilikuwa ni mimi, ndipo ungeondoa utukufu kutoka kwao. Lakini ni imani yao katika Mungu, pia, wanamwamini Mungu! Na itakubidi kuondoka, kwa imani yao. Kwa hiyo shika njia utoke hapa, na uende katika giza la nje ambako ndiko mahali pako. Nakulaani, katika Jina la Yesu Kristo, kwa mamlaka ya Biblia ya Mungu, agizo langu kwa Malaika. Sasa nenda, katika Jina la Yesu Kristo, na uwaache wawe huru. Amina.

216 Mnaadini, kwa mioyo yenu yote, kwamba mmeponywa? Inua mkono wako, useme, “Sasa namkubali Yesu Kristo kama Mponyaji wangu. Vivuli vyote vimetoweka kutoka kwangu. Sasa

ninamkubali Yeye katika ukamilifu wa nguvu Zake, katika baraka ya Uwepo Wake. Namkubali.”

Imani yangu inakutazamia Wewe,
Ewe Mwanakondoo wa Kalvari,
Mwokozi wa Kiungu;
Nisikie sasa niombapo,
Niondolee dhambi zangu zote,
Wala usiniache niondoke,
Kutoka Kwako kwenda kando.

Sasa hebu tuinue mikono yetu kwa furaha sana Kwake sasa.

Ninapotembea katika mzingile wa maisha,
Na huzuni zimenizunguka,
Uwe Kiongozi wangu (Ewe Mungu!);
Agiza giza ligeuke kuwa mchana,
Pangusia mbali majonzi, hofu,
Wala usiniache nikaondoka
Kutoka Kwako kwenda kando.

...neema tele...



MLANGO NI MWEMBAMBA SWA59-0301M
(Strait Is The Gate)

MFULULIZO WA KANISA

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, uliotolewa hapo awali katika Kiingereza Jumapili asubuhi, tarehe 1 Machi, 1959, katika Maskani ya Branham kule Jeffersonville, Indiana, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2022 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org